GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

# Mapenzi ya Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZU NO. 237 | DH.HIJ-MUHAR 1444 AH | JULAI 2023 | ZAHOOR 1402 HS | BEI TSH 800/=

# Falsafa ya Idul Adh'ha

*Shahab Ahmad, Morogoro - Tanzania*



Suala la kufurahi na kuonesha shangwe hupatikana takribani katika mila za watu wote duniani. Pengine inachukuliwa kuwa furaha isherehekewe kwa kutumia michezo, muziki, dansi na mambo mengine ya upuuzi. Lakini falsafa ya idi na kuonesha furaha iliyofundishwa na dini tukufu ya Kiislamu inaambataana na ibada, kutoa dhabihu, kumnyenyekea Allah na kuwasaidia watu wake.

Idul fitri ilianzishwa na Uislamu baada ya kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhani. Hata hivyo, kabla ya ujio wa Uislamu waarabu walisherehekea idi yao mara baada ya msimu wa Hija. Mtume mtukufu (saw) aliifanya falsafa ya idi hii iwe imeendana na dhabihu ili waislamu wapate moyo wa kujitolea.

**Mwanzo wa Idi**

Hadithi moja iliyosimuliwa na Hazrat Anas (ra) inaeleza kuwa pindi mtume mtukufu (saw) alipokuja Madina watu wake walikuwa na kawaida ya kusherehekea siku mbili za furaha na michezo. Yeye aliulizia sababu za siku hizi kuchaguliwa na akaambiwa kuwa siku hizi ziliendelea

*Ukurasa wa 7..*

# Maadhimisho ya Ukhalifa

## Majlis Ansarullah, Tanzania



*Dr. Swaleh Kitabu Pazi Sahib, (Sadr Majlis Ansarullah, Tanzania.*

Ndugu zanguni wapendwa tangu ukhalifa wa Jumuiya ya waislam wa Ahmadiyya uanze ni miaka ١١٥ sasa imefika. Sasa leo tuta angazia mambo mbalimbali yanayohusu ukhalifa. Hii ni bahati njema iliyoje sisi kuwa ndani ya neema hii ya ukhalifa na Allah ametujaalia afya njema leo tunaadhimisha na kukumbuka neema na tunahimizana ili tuendelee kuwa watiifu katika kumtii khalifa wa zama.

***1 Nini maana ya Khalifa cheo chake hadhi yake na mamlaka yake***

**Khalifa ni neno la kiarabu** lenye maana hizi kuwa **mbadala**, **mrithi, mwakilishi, Mtawala, kiongozi.** Lakini hasa hutumika katika teminilogy za kiislam kama kiongozi

# Lau Baraka na aya zinge-somwa, kungekuwa na ongezeko la Elimu

*Na.*

*Sheikh Asif Mahmood Butt Sahib*



*Endelea Uk wa 3..*

Kuhiji Bait ul Allah ...uk. wa 6

# Mapenzi ya Mungu

## Maoni ya Mhariri

# Tukienzi Kiswahili

Kwa msaada mkubwa wa Allah, tunasherehekea mwaka wa pili toka Kiswahili kipewe heshima yake na kutambuliwa na Umoja wa Mataifa. Hii ni neema kubwa kwa Tanzania na kwa kila apataye neema ni vyema kujichunguza ili aendelee kuilinda neema hiyo aliyopewa na Allah. Nini basi tunafikiri kinaweza kufanywa wakati tunasherekea mwaka wa pili wa Kiswahili kutambuliwa na kukubaliwa kimataifa?

1. Tuna wajibu wa kuzikusanya kwa umakini wa hali ya juu kazi za waandishi wetu ili ziweze kuenezwa na kusomwa kitaifa na kimattaifa Ipo miswada mingi ya washairi wazuri ambao kazi zao haziwezi kuchapwa kwa sababu wachapaji wanatawaliwa na tamaa ya fedha na sio kutunza urithi wetu. Taratibu miswada ya washairi wetu inachukuliwa na msione ajabu siku moja tukifunga safari ya kwenda kujifunza Kiswahili kwa nchi hizo za wakubwa! Tukitawaliwa na fikra za ndarahima tutadumaza lugha yetu. Yako wapi mashairi ya Palla Mlanzi Hassan, Iddi Saidi Moyoladi, Mahmoud Hamduni (Jitu Kali), Kiwato Suleiman, Mtu Kitu, Mtu Chake, Malik Abdallah Mbungiro, Khamis Sultan Wamwera, Sheikh Abdul-Rahman Muhammad Ame, Saleh Mandevu, Mtenda Mema, Ahmad Sansa Mgalaganza Tufanye hima kuzikusanye kazi hizo na kuchapisha. Tukumbuke ajizi nyumba ya njaa.

2. Ni aibu tena aibu kubwa sana tunavyojitia uzungu usio figa wala chungu. Lini tutaacha kuchanganya maneno ya Kiingereza na Kiswahili. Maradhi hayo yanashusha hadhi ya Kiswahili. Kiingereza hakina ubaya wowote. Kama unasema Kiingereza basi tumwagie kimonbokadri unavyoweza na kama unasema Kiswahili basi tupe uhondo wa Titi la Mama-Kiswahili.

3. Taasisi nyingi zinatakiwa zichukue mfano wa Mashirika ya dini ambayo usiku na mchana yanafanya kazi nzuri kuendeleza Kiswahili. Biblia Takatifu imo katika Kiswahili kizuri toka miaka mingi iliyopita. Ibada na Istilahi nyingi za kidini zimo katika Kiswahili. Jumuiya ya Ahmadiyya ambayo ilianza kazi ya mahubiri toka mwaka 1934 ni jumuiya ambayo imefanya kazi kubwa ya kuendeleza na kukuza Kiswahili. Kwa miaka yote tangu imeingia nchini imekuwa ikiendesha hotuba ya Ijumaa kwa Kiswahili, imefasiri Kuruani Tukufu kwa Kiswahili na vitabu vingi kuandikwa katika lugha ya Kiswahili. Ndio ilihamasisha kufanyika mkutano wa kwanza wa Washairi Masjid Salaam 1959. Wafuasi wa Jumuiya hii wamerutubisha Kiswahili kwa kuleta maneno haya katika Kiswahili. Sheikh Jamil Rahman Rafiq - neno Hadubini, Sheikh Kaluta Amri Abedi - Ikulu, Bunge. Kuweka Kuruani Tukufu kwenye kilele cha mlima Kilimanjaro, Jalsa Salana (Mkutano wa Mwaka), Mwana aliyeahidiwa, Siku ya Ukhalifa, siku ya waanzilishi wa dini, Mkutano wa amani - Mikutano yote hiyo wanakaribishwa wananchi wote na huanza kwa usomaji wa Kuruani Tukufu na kutolewa tafsiri ya Kiswahili kutoka hapo hufuata Shairi na hotuba zote katika mikutano hiyo inaendeshwa katika Kiswahili.

Kazi za kukienzi na kuendeleza Kiswahili ni sehemu ya mapenzi yetu kwa Taifa. Na kama alivyosema mbora wa viumbe, bwana wa daraja Mtukufu Mtume Muhammad saw kuipenda nchi ni sehemu ya Imani. Basi la kufanya hili.

*Kiswahili tukilinde, na fujo za kitatange.*
*Na nuhusi za washinde, wenye akili mawenge.*
*Kwa shauku tukipende kwa dhati tujiviringe.*
*(skaa)*




## QUR'AN TUKUFU

قَدْ صَدَّقْتَ الرُّؤْيَا ۚ إِنَّا كَذَٰلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ.
. إِنَّ هَٰذَا لَهُوَ الْبَلَاءُ الْمُبِينُ
وَفَدَيْنَاهُ بِذِبْحٍ عَظِيمٍ .
وَتَرَكْنَا عَلَيْهِ فِي الْآخِرِينَ

Umekwisha isadikisha ndoto. Kwa yakini hivi ndivyo Tuwalipavyo watendao mema.
Bila shaka (jambo) hili ni jaribio la bayana. Na Tukamkomboa kwa dhabihu kubwa. Na Tukamwachia sifa kwa watu wa baadaye.



## NUKUU YA HADITHI

**إني عند الله في أم الكتاب لخاتم النبيين وإن آدم لمنجدل في طينته، وسأنبئكم بتأويل ذلك: دعوة أبي إبراهيم، وبشارة عيسى قومه، ورؤيا أمي التي رأت أنه خرج منها نور أضاءت له قصور الشام،.**
**(المحدث: شعيب الأرناؤوط في تخريج المسند لشعيب – ١٧١٦٣ الراوي: العرباض بن سارية )**

Tafsiri: kwa Yakini mimi ni Khatam un nabiyyin mbele ya Allah Mtukufu katika ummu ul Kitab ilhali Adam alikuwa baado kuchanganywa udongo wake, nami nitawaelezeni ukweli wake. Mimi ni mwito wa babangu Ibrahim. Na bishara ya Issa kwa watu wake. Na ndoto ya mama yangu, aliyoiona kwamba Nuru imetoka kwake na ngome za Syria zilinga'a kwayo.

## Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

"Kwa hakika kulikuwa na siri kubwa ndani ya siku hiyo kwamba, dhabihu , aliyoipanda mbegu yake Ibrahim a.s. kwa siri, Mtume s.a.w. alionyesha mazao yake ya kudumu. Hazrat Ibrahim a.s.hakusita katika kumchinjia mwanaye kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Kulikuwa na somo ndani yake kwa siri kwamba mtu awe wa Mungu kwa pande zote na mbele ya amri ya Mungu, uzima wake, kizazi chake,ndugu zake na damu ya wapenzi wake, ionekane hafifu. Katika enzi za Mtume s.a.w.,aliyekuwa mfano kamili wa kila mwongozo uliotukuka, dhabihu ya namna gani ilitolewa? Pori zimejaa na damu kana kwamba mito ilitiririka na damu. Wazazi waliwaua Watoto wao, na Watoto waliwaua wazazi nao walikuwa wanafurahi kwamba kama wanasagwa katika njia ya Mwenyezi Mungu na kukatwa vipand vipande basi itakuwa raha kwao."
(Malfoozat.J.1.u.k.327 chapa ya 1988)

## MANENO YA SEYDNA AHMAD[AS] JUU YA QUR AN TUKUFU

Kurani Tukufu ndicho kitabu chenye fahari kuu kiasi hiki kwamba hapana kitabu kingine kinachoweza kuipita katika fahari yake.

Ndicho Al-Hakam, kikiwa kitabu ambacho uamuzi wake ndio wa mwisho; ndicho Muhaiman, yaani: Ni muhtasari mzima wa kila mwongozo. Ndani yake yapatikana kila hoja mtu awezayo kuhitaji.

Ni kitabu hiki ambacho kimeitimua kwa ushindi nguvu ya maadui. Kitabu kinachozungumzia kila kitu kwa undani na kinazo habari za yale yaliyokuwepo na yale yatakayo kuwepo.

Batili haiwezi kukishambulia toka mbele wala nyuma. Ndicho nuru halisi ya Mungu Mweza.

(Roohani Khazain Jal. ١٦, Uk. ١٠٣: Khutba Ilhamiya Uk. ١٠٣).

BODI YA UHARIRI

**Msimamizi:** Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
**Mhariri:** Dr. Swaleh Kitabu Pazi
**Kompyuta:** Jabiri Faraji Bishazo.
**Mchapishaji:** Sheikh Raghib Zia ul Haq
**Msambazaji:** Mwl. Omari Ali Mnungu
**Wajumbe:**
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
**Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.**
**Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.**
**Email: mapenziyamungu36@gmail.com**

# Lau Baraka na aya zingesomwa, kungekuwa na ongezeko la Elimu

*Kutoka Uk wa 1*

Sayedena Hadhrat Masihi aliyeahidiwa[as] alisema “ Islam imeweka hija ili kudhihirisha hali ya upendo. Aina zote za hofu zaonekana wazi katika nguzo za sala kwamba ina unyenyekevu mkubwa na unyonge namna gani ndani yake. Lakini njia zote za upendo zinapatikana katika Hija. Wakati mwingine katika hali ya mapenzi makubwa hata haja ya nguo pia huwa haipo. Mapenzi pia ni wazimu wa aina fulani- kujali sana nguo huwa hakupo katika mapenzi. Kwa kifupi, mfano huu wa nguo ambao hupatikana katika upeo wa mapenzi, upo katika Hija, kuna kunyolewa kichwa, kukimbia na kubusu pia- ni jambo ambalo lilipatikana katika sheria zote za Mungu kwa mfumo wa picha. Kisha umeonyeshwa upendo kamili katika kutoa dhabihu pia. Islamu imefundisha kutimiza kikamilifu haki hizi. (Al-Hakam, 24 Julai 1902 ukurasa 3)

Hadhrat Khalifa mtukufu wa kwanza[ra] alisema “ Moja ya baraka za Hija ni fundisho hili ambalo hupatikana katika nguzo zake kwamba mtu aishi maisha ya kawaida na aache kujikalifisha. Nguzo zake hupinga vikali kiburi na majivuno na hufutilia mbali uvivu na ubinafsi. Na jambo kubwa kabisa ni hili kwamba kuna mapatano ambayo yamekuwa yakiendelea kwa maelfu ya miaka nayo ni haya kuwa kwa kuhudhuria mbele ya Mungu, yeye huwa humtukuza na kufanya maombi mengi”. ( Khutbaat-e-Nur Uk 152 -Hotuba ya Idul Fitr 21 Desemba 1903)

Hazrat Khalifatul Masihi wa Pili (ra) alisema “ Hija ilifaradhishwa ili kujenga dhana ya umoja miongoni mwa Waislamu. Waislamu wote wanaojiweza hukusanyika katika Makkah kwa wakati maalumu na hivyo kila mwaka ulimwengu wa Kiislamu hupata nafasi ya kujumuika sehemu moja na hupatikana fursa ya kufikiria juu ya mahitaji yao na ya watu wengine. Lakini mbali na Hija, kuna ibada ya Umra pia ambayo haina sharti la muda wowote nayo ni ibada ya mtu mmoja mmoja. Katika nyakati tofauti mtu kila apatapo nafasi anakwenda Makkah na kutekeleza wajibu huu. Katika fundisho hili imo ishara ya kwamba ili kujenga umoja, Waislamu wanapaswa kujitolea kwa namna zote mbili yaani kwa pamoja na kwa mtu mmoja mmoja. (Anwarul Alum Jal 20, Uk 461-462)



Hadhrat Khalifa mtukufu wa tatu rh alisema “ Tukio la kweli na kuu ni Hija ambapo waislamu kutoka duniani kote huitwa kuja kwa pamoja kwa kuonyesha mfano wa umoja wa mataifa ili binadamu aelekee kwenye jambo hili kwamba sasa wakati umewadia kuwa kama vile katika mwanzo wa uumbaji wa mwanadamu ( ingawa katika sura ya kaumu ndogo ) wao waliishi kama ndugu, vivyo hivyo sasa tena mabilioni ya wanadamu waishio duniani kote waanze kuishi kama familia moja. Na minghairi ya Islamu hamna dini nyingine yoyote duniani inayoweza kujenga mahusiano haya ya mapenzi zaidi kuliko mahusiano ya damu. (Khutbaat-e-Nasir Jal 2 - 28 Nov 1969)

Hadhrat Khalifa Mtukufu wa nne rh alisema “ Sasa katika siku za Hija, zitapaa sauti kutoka dunia nzima hivyo fanyeni biashara ya mapenzi, Hija nayo ni biashara ya mapenzi. Tangu mwanzo hadi mwisho ni hadithi ya mapenzi tu ambayo itarudiwa katika Hija hii, wakiwa wamenyoa vichwa na kujifunika katika kitambaa kisichoshonwa, watu wataizunguka nyumba ya Allah bila viatu kama wazimu na watapaza sauti zao wakisema لبیک اللھم لا شریک لک لبیک لک الحمد لبیک. Hii ni biashara ya mapenzi, mandhari yote ni ya mapenzi tu. Hivyo mwisho wa dini ni mapenzi na mwanzo wa dini ni mapenzi. Mtoto akizaliwa hunyolewa kichwa na kufunikwa katika kitambaa kimoja lakini anapojaliwa kuzaliwa tena kiroho, akiwa amenyoa kichwa chake na kujifunika katika kitambaa kimoja huhudhuria mbele ya Mungu huku akipaza sauti kwa kusema لبیک اللھم لبیک . (Khutabaat-e-Tahir Jal 15, Uk 320)

Hadhrat Khalifa mtukufu wa tano aba alisema “ Mwenyezi Mungu Akielekeza kwenye ibada ya Hija Aliwaambia waislamu kwamba waelekeze fikra zao zote kwa Allah katika siku hizi kwa kuwa bila kufanya hivyo shabaha ya Hija huwa haitimii. Pamoja na hayo, pia Alisihi ya kwamba kutokana na mjumuiko mkubwa, baadhi ya maovu pia yanazuka, licha ya kwamba kutokana na mazingira ya Hija, inategemewa kutoka kwa kila mwenye kuhiji kuwa katika mazingira haya safi hawezi kufikiria chochote isipokuwa kumkumbuka Allah na kumhimidi na kumtukuza. Lakini Mwenyezi Mungu Ambaye Hujua tabia ya asili ya binadamu, Alionya kuhusu maovu matatu katika tukio hili kwamba mnapaswa kujiepusha na vitu hivyo. ( Al-Fazl International 23 Sep 2016 Uk 6 )

# Muhammad[saw]: Mfano Bora

*Kutoka Uk wa 11..*

Uingereza ambaye alifariki tarehe 27 Mei 2023. Alikuwa mjukuu wa Sahaba wa Masihi Aliyeahidiwa (as). Kwa hakika, Masihi Aliyeahidiwa (as) pia alimwona baba yake alipokuwa mdogo sana. Baba yake alikuwa Rais wa kwanza mkuu wa Majlis Khuddamul Ahmadiyya (Jumuiya ya Vijana wa Kiislamu ya Ahmadiyya). Khawaja Muniruddin Qamar alipata heshima ya kuita Adhana (mwito wa kusali) kwenye Msikiti wa Fazl nchini Uingereza wakati wa Khalifa wa Nne. Pia aliwahi kuwa Rais wa tawi la Msikiti wa Fazl na Putney. Baada ya kustaafu, alijitolea maisha yake kwa huduma ya Uislamu na alihudumu katika ofisi mbalimbali. Alihudhuria kazi ofisini hadi siku moja kabla ya kifo chake. Alikuwa na sifa nyingi na adili. Ameacha mke, watoto wawili wa kiume na wa kike wawili. Pia alikuwa mjomba wa mama wa Rais wa Taifa wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya Uingereza. Huzur (atba) alimuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu amjaalie maghfira na rehema na anyanyue cheo chake.

Dk Mirza Mubashar Ahmad ambaye alikuwa mjukuu wa Khalifa wa Pili (ra). Baada ya masomo yake nchini Pakistani, alifanya kazi kwa muda huko Rabwah, kisha akasafiri hadi London kusoma katika Chuo cha Royal cha Madaktari wa Upasuaji Edinburgh. Alikuwa amejitolea maisha yake kwa huduma ya Uislamu, na hivyo akarudi Pakistani, ambako alihudumu katika Hospitali ya Fazle Umar kwa takriban miaka 50. Pia aliteuliwa kama mjumbe wa Bodi ya Waqf-e-Jadid na Khalifa wa Nne (rh), wadhifa ambao alidumu humo hadi kufariki kwake. Siku zote aliwatunza na kuwahudumia jamaa zake. Pia alipata fursa ya kuwatumikia na kuwatendea wazee katika familia yake, pamoja na kuwatendea wengine ambao hali zao hazikuwa nzuri. Pia alitoa msaada wa kifedha kwa wasichana kupata elimu na hata kusaidia kufadhili harusi zao. Alikuwa na uhusiano wa kina na Makhalifa. Sio tu kwamba alikuwa na uhusiano na Makhalifa wakati wa uhai wake, bali daima alionyesha heshima na taadhima kubwa kwao. Khalifa mtukufu[atba] alisema kwamba licha ya kuwa na umri mkubwa, Dk Mirza Mubashar Ahmad daima alimtendea kwa heshima kubwa. Wakati wa maradhi yake ya mwisho, Khalifa wa nne[rh] alimuomba Dk Mirza Mubashar Ahmad, ambaye alisafiri mara moja kuwa pamoja naye na akabaki naye hadi kifo chake. Mara nyingi alikuwa akisafiri kwenda kumtibu Khalifa wa nne[rh] wakati wa kipindi cha ugonjwa. Inasemekana kwamba hata wasiokuwa Ahmadiyya na wapinzani wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya wangemtembelea kwa siri ili kutafuta matibabu. Kulikuwa na kijiko kidogo ambacho Masihi Aliyeahidiwa (as) angetumia kunywa dawa wakati wa ugonjwa wake. Kijiko hiki hiki kilikuja kumilikiwa na Dk Mirza Mubashar Ahmad, ambacho alikuwa akikitumia wakati fulani kwa ajili ya kupata baraka huku akiwapa dawa baadhi ya wagonjwa wake. Kuondoka kwake kumehisiwa sana na wote, waahmadiyya na wasiokuwa waahmadiyya vilevile pamoja na wafanyakazi wa hospitali miongoni mwa wengine wengi. Watu wengi walimwandikia mtukufu Khalifa (atba) juu ya mahusiano makubwa ambayo alidumisha na kila mtu. Huzur Aqdas (atba) alisema kwamba wale wanaosifiwa baada ya kufariki kwao wanaelekea Mbinguni. Khalifa mtukufu (atba) aliomba hili lithibitike kuwa kweli katika hali ya Dk Mirza Mubashar Ahmad. Huzur (atba) alimuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu amjaalie maghfira na rehema na ampe nafasi miongoni mwa vipenzi vyake.

Syeda Amatul Basit ambaye alikuwa mke wa Syed Mahmud Ahmad Basit. Alikuwa binti wa Syed Abdul Razzaq Shah na alikuwa mpwa wa Hazrat Umm Tahir. Alikuwa mara kwa mara katika kuswali, ikiwa ni pamoja na Tahajjud. Siku zote alikuwa mstari wa mbele kuwasaidia maskini. Ameacha mumewe, mtoto wa kiume na wa kike wawili. Alipendwa na kila mtu na alikuwa na mapenzi mazito kwa Ukhalifa. Hakuwahi kueleza uchungu wake mwenyewe na badala yake alijikita katika kuwatumikia maskini na wanadamu, iwe kwa kuwahudumia kimwili, kuwaombea au kutoa sadaka. Alikuwa akiomba sana na alikuwa na uhusiano thabiti na Mwenyezi Mungu. Huzur Aqdas (atba) alimuomba Mwenyezi Mungu amjaalie maghfira na rehema, anyanyue cheo chake na awawezeshe watoto wake kuendeleza urithi wa wema wake.

Sharif Ahmad Bandesha wa Faisalabad, Pakistan. Mwanawe, Rahmatullah Bandesha, ni Mbashiri. Aliwahi kuwa Rais wa Jamaat wa Jumuiya katika kijiji chake kwa muda mrefu. Alikuwa na sifa nyingi kubwa. Alikuwa na kiwango cha juu cha sala, alitumikia maskini, na alidumisha uhusiano mzuri na familia yake na wengine wote. Ameacha watoto watano wa kiume na watatu wa kike. Huzur (atba) alimuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu amjaalie maghfira na rehema, anyanyue cheo chake na awawezeshe watoto wake kuendeleza urithi wa wema wake.

# Maadhimisho ya Ukhalifa

## Jamia Ahmadiyya Morogoro, Tanzania

*Na*

**Maulana Sh. Abid Mahmood Bhuti Sahib.**

Kila ifikapo tarehe 27 mwezi wa Mei kila mwaka, wanajumuiya ya waislamu waahmadiyya huadhimisha siku adhwiim ya Ukhalifa “Jalsa Yaum e Khilafat”. Tarehe na mwezi kama huu waahmadiyya ulimwenguni kote huadhimisha siku hii kama ni moja ya siku muhimu sana katika historia ya Jamaat e Ahmadiyya, kwani tarehe na mwezi kama huu miaka zaidi ya 115 iliyopita ndipo nidhamu ya khilafat ilipoanzishwa kufuatia kifo cha mwanzilishi mtukufu wa jumuiya hii Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad as wa Qadian, kilichotokea tarehe 26/05/1908.

Khilafat ni taasisi muhimu mno kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya Islamu na inapokosekana basi hakuna chochote kinachoweza kufanyika. Kwa fadhila na baraka mahususi za Allah, Siku ya Jumamosi ya tarehe 27/05/2023 Wanachuo wa Jamia Ahmadiyya – yaani wanafunzi na wakufunzi pamoja na familia zao waliungana na waahmadiyya wote ulimwenguni kuadhimisha siku hii muhimu na adhwiim. Hafla ilifanyika chini ya uongozi wa mgeni rasmi Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhatti sahib Naib Amir na mkuu wa chuo cha Jamia



Ahmadiyya – Tanzania.

Hafla ilianza majira ya saa 4:00 asubuhi kwa usomaji wa Qurani tukufu iliyosomwa na Nasrullah Masroor Ame na kufuatiwa na shairi la Kiurdu lililosomwa kwa pamoja na Ismail A Pembe na Bashir Juma Misigo. Baada ya shairi hilo Bwana Juma Mwanyika aliwasomea wahudhuriaji nasaha mbalimbali za Hadhrat Khalifatul Masih atba alizozitoa kwa wahitimu wa Jamia Ahmadiyya Canada, Germany na Uingereza miaka ya 2018, 2019 na 2023, ambapo katika nasaha hizo Huzur atba aliwaasa wahitimu kudumisha khulka bora, kudumisha sala na hasa sala za nafali – Tahajjud, kuongeza viwango vya elimu, kusimamia vyema rasilimali za Jumuiya, kuwa na mapenzi na huruma kwa wanajumuiya n.k.

Baada ya nasaha hizo za Huzur atba, ilifuata hotuba iliyokuwa na madhumuni isemayo,”Ziara ya Hadhrat Khalifatul Masihil-khaamis atba hapa nchini na Baraka zilizoambatana na ujio wake huo – hususan kwa upande wa idara ya Jamia”. Hotuba hiyo ilitolewa na Mwl. Abdallah R Rundo sahib. Mwalimu sahib aliwakumbusha waliohudhuria mandhari ya kupendeza na shani zilizojiri wakati huo. Pia aliwaeleza wahudhuriaji ziara ya Huzur atba katika mikoa ya Mtwara / Lindi, Morogoro na Dodoma.

Baada ya hotuba hiyo ilifuata hotuba yenye anwani isemayo,”Harakati na matarajio ya Khalifa Mtukufu atba kwa Amani ya dunia”. Hotuba hii ilitolewa na Maulana Sheikh Aziiz A Shahzad sahib. Sheikh sahib alianza kwa kusema kuwa, tangu Hazrat Khalifatul Masih wa tano atba akalie kiti cha Ukhalifa amefanya juhudi kubwa sana ili kuipatia dunia Amani ya kweli. Akigusia juhudi hizo, alisema kuwa ni pamoja na kukutana na viongozi mbalimbali na kuwapatia ujumbe wa Amani, kuhotubia Bunge la Ulaya na kuwafikishia ujumbe wa Amani, kuwaandikia barua marais wa Urusi, Marekani, Ufaransa na Iran na pia kuwaandikia mawaziri wakuu kadhaa akiwemo wa Uingereza na wa Israel na Chancelor wa Ujerumani. Haya yote yathibitisha wazi kuwa Khalifa wa zama anajihusisha zaidi na ustawi na Amani si tu kwa wafuasi wake, bali wanadamu wote kwa ujumla. Sheikh sahib alimaliza kwa kunukuu maneno ya Hazrat Masihul-Mau’d as pale anaposema,’ Njooni kwangu mkapate utulivu kwani mimi ndimi boma la Amani”.

Baada ya hotuba hiyo, zilifuata nasaha maalum za mgeni rasmi ambaye kwa hakika alizungumza mengi yaliyobeba ujumbe mzito kwa wahudhuriaji. Alisema kuwa sisi tuliopo katika idara hii ya Jamia ndiyo mashuhuda wakubwa wa Baraka za ziara ya Huzur atba. Alisema alifika hapa nchini takriban miaka 17 iliyopita na hali ya Jamia aliyoikuta wakati ule ni tofauti sana na ya hivi sasa na watu wote waliyoiona wakati ule bila shaka wanakiri juu ya hili. Aidha aliwakumbusha wahudhuriaji juu ya jukumu muhimu sana la kuulinda Ukhalifa, amesema kuwa jukumu hili halihitaji silaha nzito nzito bali ni kwa njia ya sala, ikuwe sala ya Tahajjud maombi mengi yenye ikhlaas na kudumu katika maombi mengi na khulka njema. Mwisho aliongoza maombi ya kimya na kufunga hafla.

# Maadhimisho ya Ukhalifa

## Majlis Ansarullah, Tanzania

*Kutoka Uk wa 1*

wa waislam wote duniani ambaye huchukua nafasi ya Mtume aliyefika katika zama husika. Kama vile alipofariki Mtume Muhammad saw walifuata warthi wa kiti chake ambao waliitwa makhalifa kwa maana ya cheo walichopata baada ya mtume. Khalifa ni kifupi cha neno Khalifatu rasuulullah saw, lenye maana ya makamu wa Mtume saw katika Umma wa waislam.

***Na hizi ndiyo istilahi za kiislam***

Pia allama Baidhawii anasema kwamba’’ الخَلِيفَةُ مَنْ يُخْلِفُ غَيْرَه، وَيَتُوبُ مَتَابَه ( تفسير بيضاوى جلد ١ صفحہ ٥٩)

***Yaani khalifa ni yule anae kuja baada ya mwingine nae anakuwa mrithi wake***. [Tafsiri baidhawii Jalada la 1 ukurasa wa 59]

Pia Allama Ibni Athiir anasema kwamba’’

الْخَلِيفَةُ مَن يَقُومُ مَقَامَ الذَّاهِبِ وَيُسَمُّ مَسَدَّه ( النهاية جلد ١ صفحه ٣١٥

***Yaani khalifa ni yule anae simama mahala pa yule aliye ondoka na kujaza nafasi iliyoachwa wazi.*** [Annihaayatu Jalada la 1 ukurasa wa 315]

***Mamlaka ya khalifa***

Mamlaka ya khalifa ni makubwa kwa sababu anamuwakilisha mtume na hupewa muongozo na Allah juu ya mambo mbalimbali anayofanya au yanayotokea na akiwa hapati jibu la haraka. Pia khalifa katika wakati Fulani anaweza kuwa na mamlaka ya kiserikali kama ilivyo kuwa kwa makhalifa wa Mtume saw kwani hata yeye Mtume alikuwa na cheo cha utume na pia alikuwa na cheo cha ufalme kama serikali kwasababu aliongoza watu wote wenye dini na wasio na dini Waislam na wasio kuwa na uislam, alipofariki yeye basi makhalifa wake wakarithi mamlaka hayo ya kuwa makhalifa na kuwa Wafalme.

**2 Je makhalifa walipatikana katika Islam?**

*Hdithi hizi zinaonyesha wazi kwamba ukhalifa ulipatikana ndani ya Islam, maana mtume saw alisema kuwa”*

عَلَيْكُمْ بِسُنَّتِي وَسُنَّةِ الْخُلَفَاءِ الرَّاشِدِينَ الْمَهْدِيِّينَ «
(ترمذى كتاب العلم باب الاخذ بالسنة ابو داؤد كتاب السنة باب لزوم السنة).

*Enyi Waislamu! Ni wajibu wenu kufuata Sunnah zangu na sunna za makhalifa wangu waongofu.*

Mtume Muhammad[saw] akasema kuwa’’

الخِلَافَةُ ثَلاثُونَ عاماً ثُمَّ يَكُونُ بَعْدَ ذَلِكَ الْمُلك
(٢٢٠ صفحه ٥ جلد احمد مسند )

Yaani ukhalifa uliowekwa baada yangu utadumu kwa miaka arobaini kisha kutakuwa na kipindi cha ufalme.

*Uteuzi wa Mtume na Khalifa*

Inafaa kutambua kwamba mifumo miwili ya Utume na ukhalifa imetoka kwa Mwenyezi Mungu mwenyewe, lakini kuna tofauti katika majukumu yake. Utume unakuja wakati ule dunia imejaa ufisadi na uasi, Shirki na giza la imani lipo kila mahali. Hivyo kwa wakati kama huo, uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu hudhihirika katika mfumo wa kuleta utume duniani. Pia kwa upande mwingine, uwezo wa Allah mtukufu hudhihirika kwa namna ya ukhalifa kwa maana ya kudra ya pili ambapo Jamaati iliyoanzishwa na Mtume ambayo inatimiza masharti ya imani na matendo mazuri lina pata kiongozi toka miongoni mwao ili kutimiza bishara na matakwa ya Mwenyezi Mungu ambayo hayakutimia wakati wa uhai wa Mtume.

Na hii ndiyo sababu ya kuwepo tofauti katika njia ya kumchagua Mtume na Khalifa. Mtume anachaguliwa moja kwa moja na Mwenyezi Mungu, kwa sababu katika kipindi hiki cha giza, mkusanyiko wa waumini haupatikani, na baada ya kuja kwa Mtume, umati wa waumini unaundwa, na baada ya kifo cha Mtume, Mwenyezi Mungu kwa upendeleo wake, anaweka mfumo wa ukhalifa katika mkusanyiko huu wa waumini. Na umma huo wa waaminio unatimiza masharti ya imani na matendo mazuri kwa njia inayomridhisha Mwenyezi Mungu.

**Hakika swali hili lipo wazi kabisa** kwa kila mwislamu **kwamba Makhalifa walipatikana katika Islam** na kwa idadi yao walikuwa wanne tu baada ya kifo cha mtume saw lakini kuna bishara ya kupatikana tena katika zama za mwisho.

***Nitawataja hapa pamoja na zama walizodumu katika uongozi au kiti cha ukhalifa***

**Hadhrat Abubakar Swiddiq r.a aliongoza katika kiti cha ukhalifa toka tarehe 8 June mwaka 632 hadi tarehe 23 mwezi wa tisa mwaka 634. Yeye alizaliwa tarehe 27 / 10 / 573 na akafariki tarehe 23 mwezi wa tisa mwaka 634 akiwa na umri wa miaka 60.**

**Hadhrat Omar Bin Khattab r.a aliongoza toka tarehe 23 mwezi wa tisa mwaka 634 hadi tarehe 3 / 11/ 644. Yeye alizaliwa mwaka 582 au 583 sawa na tofauti za kihistoria**

*Endelea Uk wa 8...*

# Kuhiji Bait ul Allah



Na **Sheikh Karimuddin Shams**
Morogoro, Tanzania

## Ishara Kuu ya Mungu Mmoja

Maelezo ya kina juu ya Maamrisho ya Hijja
Kutoka kwa hazrat Musleh Maud[ra]

**وَأَذِّن فِي النَّاسِ بِالْحَجِّ يَأْتُوكَ رِجَالًا وَعَلَىٰ كُلِّ - ضَامِرٍ يَأْتِينَ مِن كُلِّ فَجٍّ عَمِيقٍ**

**لِّيَشْهَدُوا مَنَافِعَ لَهُمْ وَيَذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ فِي أَيَّامٍ- مَّعْلُومَاتٍ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُم مِّن بَهِيمَةِ الْأَنْعَامِ ۖ فَكُلُوا مِنْهَا وَأَطْعِمُوا الْبَائِسَ الْفَقِيرَ**

**ثُمَّ لْيَقْضُوا تَفَثَهُمْ وَلْيُوفُوا نُذُورَهُمْ وَلْيَطَّوَّفُوا بِالْبَيْتِ الْعَتِيقِ**

(Al-Hajj-27-29)

Tafsiri; Na uwatangazie watu kwamba waaje kwako kwa nia ya kufanya Hijja, wakufikie kwa miguu na juu ya kila mnyama mkondefu, wakija toka kila njia ya mbali. Ili washuhudie manufaa yao na kulitaja jina la Allah, katika siku maalum,juu ya yale aliyowaruzuku katika wanayama wenye miguu minne.na kuleni katika hayo na mlisheni mwenye shida, fakiri. Kisha wajisafishe uchafu (wa maovu) yao, na watimize nadhiri zao, na wazunguke Nyumba ya Kale (yaani Baitullahi Al-ka'aba).

Wasomaji wapendwa wa gazette la Mapenzi ya Mungu! Tunakuleteni ufafanuzi mtamu wa hazrat Musleh Maud r.a. khalifa wa pili wa hazrat Masihe Maud a.s.kwenye kurasa hizi ili muweze kupata hadhi na utamu wa maelezo ya Kurani Tukufu hivyo muyasome kwa umakini mkubwa. Jazakum ul Allah mtukufu. (Karim ud din Shams).

Hazrat Musleh Maud[ra]. anasema: " Allah Taalah Anasema kwamba, tulimwambia Ibrahim kuwa, amri hii haikuhusu wewe tu bali ni kwa ajili ya wanadamu wote kwamba watu wakufikie toka kila njia ya mbali juu ya wanayama waliokonwa kutokana na safari ndefu ndefu za kufikia huko kupitia njia zilizochimbika na kuharibika kabisa kwa sababu ya kutumika sana, ili wapata manufaa ya kidunia pia na kumkumbuka sana Mungu katika siku maalum, hivyo dini moja tu ipate kustawi duniani kote. watajiri wenu wanapaswa kula wenyewe katika nyama ya dhabihu na kuwalisha maskini pia kisha wapate kuoga baada ya kuchinja dhabihu na kujisafisha uchafu wao yaani wajisafishe kidhahiri na kiroho pia na kuuondoa uchafu wa mioyo yao. Na kutimiza ahadi walizozifunga na Allah na kuhiji nyumba hii ya Kale ya Ibada.

Isieleweke na hilo kuwa kitu kisicho na uzima kimepewa cheo cha kiungu bali uzungukaji wa Ka'aba ilikuwa desturi ya zamani kama alama ya kutoa dhabihu. Watu walikuwa wanazunga kwenye wagonjwa kwa maana ya kuwa tujitolee kwao ili wao wapate kusalimika. Imedokezwa hilo tu ndani ya aya hii kwamba watu wataendelea kupatikana ambao watadumu katika kujitolea uzima wao kwa ajili ya adhma na ibada ya Mwenyezi Mungu, waila kuzunguka kidhahiri haina uzito wowote wenyewe.

Mwenyezi Mungu Ametaja uzungukaji Ka'aba ndani ya aya hizo, iliyoibada muhimmu ya Kiislam, , ila leo kila mmoja wao analainisha ulimi wake na Allahu Akbar, Allahu Akbar, Lailaha Illahu, Allahu Akbar wa Lillahil hamd. Na kuendelea kutamka Labbaik Allahuma laka Labbaika, La Sharika laka Labbaika, kana kwamba Mungu Yuko Amesimama mbele ya macho yao, Nao wanamwambia kuwa Ewe Mola wetu tumeshafika kwako, tunakiri kwamba hakuna mshirika wako, wewe tu unayestahili kuwaita watu kwako, na ewe Mungu tumeshakuja kwako kwa kuutikia mwito wako, basi mji wa Makka ni



kutokanayo,kila mwaka malukuki ya watu, ambao wanatofautina kitaifa, mila na nchi hata kilugha na ada, wanakusanyika Makka tukufu na kukiri kwa kitendo chao kuwa Umoja wa Kiislam umeshaunganisha nyoyo za Waislam kiasi hiki kwamba wako tayyari kujumuika pamoja katika sehemu moja wakiitikia sauti ya Mungu pasipo hitilafu zao za kilugha, kitikadi, kirangi, kimila, kimawazo, na ya kimazingira. Hali kadhalika Waislam wameshathibitisha kivitendo pamoja na kuzunguka Ka'aba kidhahiri kwamba, wako tayyari kwa ajili ya kutoa dhabihu ya uzima wao kwa ajili ya Kuilinda Ka'aba na maadamu roho hii itapatika kwa Waislam hakuna adui atakayekuwa na uwezo wa kuelekea kwenye Ka'aba au kuharibu umoja wao kwani maadamu Ka'aba ipo umoja wao pia utakuwepo. Si tu kwamba wanakuwa na mtazamo huu mbele ya macho yao kwamba Mwenyezi Mungu Ameshasambaza Islam kwenye kona zipi na zipi za dunia na juu ya hilo wanaona pia kuwa sauti iliyotoka kutoka jangwa lisilo na maji wala chakula, lisilosikika hata na watu wake,bali walikuwa wanamtesa na kudhulumu mwenye sauti lile, leo hii imeshafika kwenye kona zote za dunia na kuwakusanya pamoja malukuki ya watu. Wao wanashuhudia ishara hii kubwa ya Mwenyezi Mungu na kupata kuhuika kwa Imani kwamba Mtume Muhammad[saw].alizaliwa aliyetangaza sauti iliyopata kusikika sana na kuendelea kusikika hadi kufika kwenye nchi za mbali na kuwavuta watu hadi kuwaleta huko. Na ule Makka ambao udhia, shida na taabu za ahali zake ziliwalazimisha Waislam ili waache nchi yao nao hawakuwa na ruhusa ya kutamka La Ilaha Illallahu mahala ambapo malukuki ya Waislam wanajumuika ili kumuabudu Allah Mtukufu na kutoa ushuhuda mbele ya dunia kuwa dini iliyoletwa na Muhammad saw Mjumbe wa Allah iko hai hata leo na watumishi wake wapo duniani kote kwa ajili ya kuitangaza sauti yake ina maana Hijja inatngaa ujumbe huu kwamba damu ya uhai ipo kwenye mishipa ya Islam. Watu wanompenda Muhammad, mjumbe wa Allah wamekusanyika hadi sasa katika makao mkuu ya Kiislam na kuutangaza undugu ule unaopatikana kati yao na kati ya Islam na Muhammad saw mtume wa Mungu. Nao hutoa ushuhuda huu kwamba watu wanaoipa jina la Muhammad saw wanapatikana duniani hadi sasa na maendeleo yao ya kitaifa yanakuwepo kwa sasa pia, …, Islam jinsi ilivyofaradhisha sala, saumu na zaka vivyo hivyo imelazimisha Hijja. Bila shaka kusudio la kiasili la kiroho la Hijja ni kufungamana na Allah kwa moyo wote kwa kavunja uhusiano wowote ule lakini Mwenyezi Mungu Ameilazimisha Hijja pia kidhahiri ili kutimiza shabaha hilo na kuwafaradhishia wenye uwezo kuenda kuhiji Ka'aba wakiziacha nyumba zao na kujifunza somo la kujitolea kwa ahali na nchi zao kwani Islam inakubali umuhimmu wa kiroho amoja na mwili. Kama kidhahiri, kila mtu anakuwa na mwili wake hapo duniani na kuwa na roho ndani yake hali kadhalika dini na Roho pia inakuwa na miili zake zinazotakiwa kuzishikilia…..ni wazi kabisa kuwa lengu kuu la Maisha ya binadamu ni kumuabudu Allah na kupata ukaribu naye, kama Alivyosema Mungu… nimemuumba binadamu ili apate ukaribu nami basi Hijja ni alama ya jambo hilo ya kwamba shabaha ambalo ameumbwa binadamu kwalo, ameshalitimia. Au kwa maneno mengine tunaweza kusema kwamba Hijja ni nini? Kupata kumwona Allah na kumshuhudia(kupitia kudra zake). Ila, Mwenyezi Mungu Ameweka mwili kidhahiri kwa ajili ya shabaha hiyo ili roho pia ipate kulindwa kuupitia mwili.

Kisha Hijja inahuisha tukio lile la uaminifu wa kweli ambalo mfano wake ulioneshwa na hazrat Ibrahim kabla ya miaka elfu nne hivi tokea leo na matunda yake yanashuhudiwa na dunia hadi sasa.( kwamba hazrat Ibrahim alipomuacha mkewe na mwanaye jangwani kwa amri ya Allah Mtukufu basi Mwenyezi Mungu Alidhihirisha kudra yake na kuonesha muujiza mkubwa na kuwapatia mahitajio yao yote huko huko jangwani n.k.)

Hadi leo kwa kukumbuka tukio lile la bi Hajira r.a. (pale alipozunguka kwenye milima wa Safa na Marwa) kila mwenye kuhiji anazizunguka zile milima miwili mara saba. Kutembelea huko kunathibitisha kufuata nyayo za Bi Hajira na kutangaza kuwa sisi kama tutalazimika kuwaacha watu wetu na ahali zetu kwa njia ya Mwenyezi Mungu basi hatutasita kufanya hivyo.

Basi hijja ni ibada muhimmu sana iliyolazimishwa na Islam. Mtu yeyote anapokuwenda Makka na kutekeleza kikamilifu ibada za Hijja basi anashudia kwa dhati yake jinsi wanavyopata uhai wa kudumu milele wanaojitolea kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

Kisha roho ya umoja pia inazalika ndani ya waislam kwa Hijja na wanapata kutafakari juu ya mahitajio yao na ya wengine pia, hivyo wanapata nafasi ya kushuhudia sifa nzuri za wengine na kujifunza kwao na kuongezeka katika kuelewana na kupendana. Hivyo basi Hijja ni nguzo muhimmu mno kati ya nguzo za Kiislam ambayo watu wamehimizwa kwayo na Islam na watu ambao wamepewa uwezo wa mali na Allah nao wana afya ya kuvumilia shida za safari, wanawajibika kutekeleza amri hii na kujinufaisha na baraka za kuhiji Bait ul Allah. Ninahisi kwamba wema mkubwa kwa ajili ya watajiri siku hizi ni kufanya Hijja…

Bila shaka, hijja ni wema mkubwa lakini kama yeyote anafanya Hijja ili apate heshima kwa watu au anatekeleza ibada hii kwa ajili ya mazoea tu au anafanya Hijja ili aitwe al-haji basi anaweza kupoteza Imani yake ya mwanzo pia aliyokuwa anayo hapo awali…basi kuhiji inafaa pale tu ambapo mtu anakuwa na hofu ya Mungu moyoni mwake na kuitektleza faradhi hii kwa uaminifu na upendo na kama anakoenda kwa uaminifu basi hurudi na marundo ya Imani.

(imechukuliwa kutoka Tafsir e Kabir J.6 chin ya aya 28-30 za sura Al-Hajj: Karim Uddin Shams)

# Bustani ya Washairi

## Haki sawa ndio nini

Haki sawa ndio Nini, naomba munieleze
Kila Kitu kiwesawa, maumbile tusawaze?
Majukumu yawesawa, Wana tuwanyonyesheze

Haki sawa ndio Nini, naomba munieleze?
Kulima tufanye sawa, kupika nakozamuze
Sauti zipande sawa, siwepo naapunguze

Haki sawa ndio Nini, naomba munieleze
Auviti viwesawa, vyeo tukigombeaze
Wasosifa kiusawa, mamlaka tuwajaze

Haki sawa ndio Nini, naomba munieleze
Baba mama wawe sawa, sauti tuzipuuze
Nayemama awesawa, ubini tumuitize

Haki sawa ndio Nini, naomba munieleze
Au ndoa ziwesawa, mke namke tuoze
Wanaume naosawa, mume kwa mumetuoze

Haki sawa ndio Nini, naomba munieleze
Mabingwa wahaki sawa, kinyume munieleze
Hukunaku kuwe sawa, mlingano idadize.

Mtunzi
M.O.kisagwa

## Usikatae Mitala

Mjenzi ndiye mjuzi, kwakile alokiunda
Aloijenga kurunzi, mbali sana akakwenda
Akiba akamaizi, vifaa akaviunda
Usikatae mitala , mjenzi ndiye mjuzi

Hebu mwangalie kuku, jogoo alokomaa
Matembe wenyeshauku, dhamana humpatia
Waamsha mwanzo siku,namwewe kuwaambia
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi

Muumbaji anajua, ndiyo mana akasema
Rukisa wewe kuoa, wanawake walowema
Moja Hadi nne oa, kuzidisha sio wema
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi

Akili yako tumia, mitala ukizuia
Wale wanaobakia, utawa watatulia??
Kama hawatatulia, Nini Sasa chafwatia??
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi.

Akili yako tumia, Nini kitachotokea
Usawa tukitumia, mitala kwa mke pia
Mimba mke kipatia, baba yupi atalea
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi.

Kumbuka nakuambia, Kila mwana anababa
Jini wanazichangia, nusu mama nusu baba
Ugomvi utauzua, kugombania ubaba
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi

Hayo Kenda nakwambia, kumi hili lisikia
Siku zikishakujia, au mwana ukazaa
Waume tavumilia??au dhambi tawatia
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi.

Mtunzi
Masihi omary stambuli kisagwa

## Wako wapi?

Baliwa waliotamba, bila wao hatushindi.
Mitaani wakiyumba, na kupita kwa makundi.
Wamekuwa ni wembamba, kusagika ja mahindi.
Masikini Binadamu, mwepesi wa utelezi.

Mahmood Hamsin Mubiru (wa Mamba)
Migombani-Kiwalani.

## TUSIZIBEZE KUFANYA-SHUGHULI ZA JAMAATI

NIDHAMU kitu azizi, kwenye wowote Umoja
Muhimili na mizizi, wa kile mlichochuja
Kitaenziwa makuzi, na kuendeshwa kitija
Shughuli za Jamaati, tusizibeze kufanya.

Kwenu wanajamaati, majina sita yataja
Bali nyote jumlati, ipokeeni lihaja
Waume na mabinati, wito huu unakuja
Tusizibeze kufanya, shughuli za Jamaati.

Wote ninawashauri, NIDHAMU kutoifuja
Bila hiyo ni khatari, bila hiyo kifo chaja
Hivyo kwa kujinusuri, tuwe nayo bila hoja
Shughuli za Jamaati, tusizibeze kufanya.

Huusikiapo wito, waitwa kwenye shughuli
Kusadi wajawazito, ama Wakala-Amali
Itika siwe mzito, wala kuuliza swali
Tusizibeze kufanya, shughuli za Jamaati.

Jua sisi wanajeshi, wakati wote kazini
«Leo ni vipeperushi», tunavigawa mjini
Tusitengeneze shushi, haipo kwenye kanuni
Shughuli za Jarmaati, tusizibeze kufanya.

Huhimizwapo kutoa, katika njia ya Mola
Mazao mifugo pia, wakadhaa kawarila
Uache kulimatia, toa upate fadhila
Tusizibeze kufanya, shughuli za Jamaati

Tunyoshe mikono yetu, viganja tusivifumbe
Tuzitoe mali zetu, Kondoo, Mbuzi na Ng›ombe
Ikibidi kila kitu, si vyetu ni vya Muumba
Shughuli za Jamaati, tusizibeze kufanya.

Patamkwapo twendeni, twendeni hospitali
Wagonjwa tuwaoneni, tukawajulie hali
Acha sababu kubuni, shiriki katika hili
Tusizibeze kufanya, shughuli za Jamaati

Na mmoja kati yetu, maradhi yakimpata
Wallahi tusithubutu, bila ya kwake kupita
Huyu ndiye ndugu yetu, tusimwache katakata
Shughuli za Jamaati, tusizibeze kufanya.

Tukamjulie hali, kama tunacho tumpe
Aende hospitali, gharama dawa alipe
Ndio udugu wa hali, na mali tusiutupe
Tusizibeze kufanya, shughuli za Jamaati

Tamati twakumbushana, unafaa ukumbusho
Hasa kwa wauminina, twafanya masahihisho
Tujisahihishe sana, tushike safi fundisho
Shughuli za Jamaati, tusizibeze kufanya

***Al-Ustadh Mhenga***
***Khamisi S. S. Wamwera***
***Kimbangulile - Mbagala Rangitatu.***
***Dar es Salaam.***

## DHAHABU YA KUSINI:

Nakuomba Maulana, uniongoze
Nikiwa bado kijana, nijitulize
Nifanye vyenye maana, nisizogoze
Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

Sina uwezo wowote, wa kuilinda
Itanibidi nijute, ikinishinda
Sijivunii chochote, nisijekonda
Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

Ikitokeza juani, yameremeta
Inawindwa na wahuni, wapiga ngeta
Nikisema kulikoni, wananipeta
Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

Nikihifadhi kizani, yametameta
Wanasema hiko nini, yamenikuta
Ninajishika kichwani, nasikitika
Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

Ninakuomba Rabana, unilindie
Si usiku si mchana, iangalie
Mana inang'ara sana, isipotee
Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

Kuomba siwezi acha, maisha yangu
Hata kama kumekucha, kanuni yangu
Na mimi sio ndondocha, imani yangu
Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

Mungu wangu Mungu wangu, unibariki
Bado naona uchungu, wa wazandiki
Bado Dhahabu ni yangu, wanahamaki
Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

Bado ninaifunika, isiponyoke
Watu wataka ipoka, waburudike
Kukuomba sijachoka, unikumbuke
Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

Sina ujanja wowote, wa kuitunza
Na wahuni kama wote, wataniponza
Ninafata njia zote, za kuitunza
Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

Dhahabu ninayo ndogo, siipotezi
Vijana hawana dogo, wana uchizi
Wasije nipa kisago, cha upekuzi
Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

Ngoja wapate za kwao, washuhudie
Leo kwangu kesho kwao, wasijutie
Hii yangu sio yao, wasiumie
Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

Shida yenu ipo wapi, inashangaza
Ni Dhahabu sio pipi, ninawajuza
Vya watu hamuogopi, mnajiliza
Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie.

Sina ujanja wowote, wenye kiburi
Kukuomba kama kote, ndio Kahari
Nangu mipa si chochote, si mtabiri
Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

Nitunzie hii kitu, nijivunie
Mimi hapa kama mtu, nikumbatie
Na roho zao za kutu, wahurumie
Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

Kwa leo ninasitisha, nimekomea
Misuli nimetunisha, najihemea
Sio kama nawatisha, mtapotea
Rabbi taqabbal Du'a, nihurumie.

Abdallah Kalindima
#CHUMACHAKAVU
Kalindimasenior@gmail.com

# Falsafa ya Idul Adh'ha

*Kutoka Uk wa 1..*

kusherehekewa katika mila za watu katika zama za ujinga. Mtume mtukufu saw akasema kuwa sasa Mwenyezi Mungu amewapa siku mbili nyingine ambazo ni bora zaidi na zina falsafa nzuri kuliko hizo walizokuwa wakizifurahia. Hivyo, waislamu walianza kusherehekea Idul fitri na idul Adh'ha baada ya kuhamia Madina.

**IDUL ADH'HA**

Idul Adh'ha au idi ya dhabihu husherehekewa kwa kumkumbuka Nabii Ibrahim (as) alipoamua kumchinja mwanaye Ismail baada ya kupata mwongozo katika ndoto. Kurani tukufu imetumia neno la dhibhin adhim yaani dhabihu tukufu kwa ajili yake na maelezo yake yametunzwa ndani ya sura As-saafaat sura ya 37. Waislamu duniani kote huchinja wanyama siku hiyo ya idi ili kukumbuka tukio hili na pia kuonesha kwamba wako tayari kujitoa mhanga.

**YOUM UN NAHR**

Siku ya kuchinja yaani youm un nahr ni kilele cha Hija. Hija ni nguzo ya tano katika Uislamu. Hija ina mambo matatu ambayo ni faradhi:

- Kuvaa ihramu
- kukaa Arafat ambayo ni tarehe 9 dhulhija.
- tawaf yaani kuizunguka Kaaba ambayo hufanyika tarehe 10 dhulhija.

Mambo mengine pia ni sehemu ya Hija kama vile kukaa katika Mazdalifa, Sai'i yaani kukimbia kati ya vilima viwili Safa na Marwa, Ramiul Jimar yaani kurusha mawe au kupiga vijiwe, kuchinja mnyama, kunyoa nyewele na kuzunguka tena.

**YOUM UL ARAFAT**

Youm ul Arafat au siku ya arafa ina umuhimu wake. Imesimuliwa na Bi Ayesha (ra) kwamba Mtume mtukufu (saw) alisema kuwa siku ya arafa Mwenyezi Mungu hunusuru watu wengi kutoka motoni zaidi kuliko siku nyingine. Siku hiyo anawaamuru malaika kuwapatia watu wake yote wanayoipenda.

Vivyo hivyo, Mtume mtukufu (saw) alieleza umuhimu wa Youm un nahr (siku ya kuchinja) akisema siku hii ni ya Haj-i-Akbar au Hija kubwa.

Siku ya idi ni siku ya furaha kwa waislamu wote. Ndiyo maana Mtume mtukufu saw) alikataza kufunga saumu katika siku za idi. Yeye mwenyewe alikuwa na Sunnah ya kuacha kula asubuhi ya idul Adh'ha na alikula katika nyama ya dhabihu aliyemchinja mara baada ya Sala ya idi kama kitu cha kwanza kula siku hiyo.

**MAANA YA HIJA**

Neno Hija maana yake Kasd yaani kusudio la kupata kitu na katika maana ya kiroho huonyesha safari ya kutoka ka- tika dunia kwenda kwa Mwenyezi Mungu na kuungana naye.

Kwenda kuhiji Makka ni ishara ya kupafanyia heshima mahali palipodhihirika nia ya Mwenyezi Mungu na tendo hili linafanya kazi ya kuwakumbusha waaminio matukio hayo. Hukumbusha habari ya Nabii Ismail na mama yake Hajirah walioachwa na Nabii Ibrahimu jangwani na kukumbusha jinsi wanavyokuzwa na kuheshimiwa watu wanaotoa sadaka katika njia ya Mwenyezi Mungu; jambo hili huingiza katika roho ya haji imani idumuyo kuamini nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu. Hujiona yupo karibu na mahala palipowekwa kwa ajili ya kumwabudu Mwenyezi Mungu Mmoja wa Kweli tokea zamani zisizojulikana na anaona kuwa ameunganika kwa kiroho na watu ambao kwa karne nyingi zisizohesabika wameunganishwa pamoja kwa kumpenda Mwenyezi Mungu na kumkumbuka naye mwenyewe hujihesabu miongoni mwao.

**DHABIHU**

Dhabihu za siku ya Idul Adh'ha hutufundisha kujitolea kwa ajili ya watu wengine. Jumuiya ya Ahmadiyya ni kinara katika kuwasaidia watu maskini na wasiojiweza. Hivyo, falsafa ya Idul Adh'ha imebebwa vizuri ndani ya Jumuiya.

Hazrat Khalifatul Masihi wa Pili (ra) alisema:

Idi ya leo inaitwa Idul Adh'ha yaani idi inayohusika na dhabihu. Idi hii huangukia siku ya pili ya Hija kana kwamba imeambatana kabisa na Hija. Madhumuni ya kuisherehekea ni kukumbuka dhabihu ya Nabii Ibrahim aliyoitoa mbele ya Mola wake. Hivyo, idi hii ni kumbukizi ya kujitoa mhanga kwa Nabii Ibrahim ya kwamba alikuwa tayari kumchinja mwanaye kwa ajili ya Allah.

(Khutbaat e Mahmood, juz. 2, uk. 244)

**FALSAFA YA IDUL ADH'HA**

Hazrat Masihi aliyeahidiwa[as] Kwa hakika siri iliyopo ndani ya siku hii ni kwamba mbegu ya dhabihu iliyopandwa na Nabii Ibrahim[as] kwa kuficha basi Mtume Muhammad[saw] alionesha mazao yake mazuri. Nabii Ibrahim[as] hakuona wasiwasi katika kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu ya kumchinja mwanaye. Humo ilikuwa ni ishara hii kwamba mtu awe wa Mwenyezi Mungu kikamilifu na mbele ya amri ya Mwenyezi Mungu uhai asione hata uhai wake au damu ya watoto wake na jamaa zake, kuwa haina maana.

(Malfuzat, juz. 1, uk. 327)

**SABABU YA KUSHEREHEKEA IDI**

Hazrat Musleh Ma'ud (ra) akieleza hekima yake anasema:

"Mwislamu wa leo anaposherehekea Idul Adh'ha basi sababu yake haiko kuwa Mwenyezi Mungu alimnusuru Nabii Ismail au kwa sababu Nabii Ibrahim hakukosa imani na kwa mujibu wa amri ya Mwenyezi Mungu alikuwa tayari kumchinja mwanaye; bali waislamu kila wakusanyikapo kwa ajili ya idi hushuhudia jambo hili kwamba utabiri huu ulitimia sawasawa kuwa idadi ya nyota

*Endelea Uk wa 9..*

# Maadhimisho ya Ukhalifa

## yafana Mkoani Ruvuma

*...Kutoka toleo lililopita*

wafananisha na wale wa kabla yao ambao walifanywa makhalifa wakati walipo mwamini Allah na wakafanya vitendo vizuri.

**Atawaimarishia dini yao aliyowapendelea.** Dini inayo zungumzwa hapa na Allah ni Islam kwasababu Allah anasema katika sura ya 5 aya yake ya 4 kuwa leo nimewakamilishieni dini yenu na kuwatimizieni neema yangu na nimewapendeleeni Islam iwe dini yenu. Sasa khalifa ambaye Mwenyezi Mungu anatoa ahadi kaziyake kuja kuimarisha dini hii ya Islam na sio dini nyingine. Hivyo waislamu wote wanatakiwa kufuata amri hii ili ahadi hii itimie kwao kwa sababu Allah kamwe Hatoi ahadi isiyoweza kutimia.

**Atawabadilishia amani baada ya hofu yao,** kwanza kabisa tujue kuwa hofu huwa haipatikani wakati watu wako na Amani hofu huja pale kitu ukipendacho kikiondoka ghafla, mfano anapo fariki mzazi au mke au yule mtu ambaye katika maisha haya ya dunia mlishibana sana. **Hivyo kwa upande wa waislam masahaba r.**a walimpenda sana mtume Muahammad saw na waliposikia amefariki tu wengine hawakuamini na kulia sana ,mfano wao Hasan bin Thabit[ra] mwingine Hadhrat Omar Bin Khattab[ra] Mfano huu wa Hadhrat Omar[ra]. ulikuwa ule ambao unaonyesha jinsi gani alivyokuwa na khofu na hakujua afanye nini muda ule, ndipo Mwenyezi Mungu alipo muinua Hadhrat Abubakar swddiq r.a na kuwasomea aya inayo eleza kifo cha mtume na kuwaeleza anae mwabudu Muhammad ajue huyo amesha kufa na anaye mwabudu Allah basi ajue Allah yu mzima na Hafi. Hapo hofu walio kuwa nayo muda ule ikatoweka yote na Amani ikapatikana na islam ikaendelea kushinda chini ya kiongozi huyu yaani Hadhrat Abubakar[ra]. **Sasa hofu ya pili inakuja kwetu sisi wa zama hizi kwa kuona uislam unashambuliwa na waislam wamegawanyika na hatujui tuta jibu nini au tutaeleza na kuusafisha vipi Uislam na masingizio**. Walipatikana watu wachache wenye yakini kwa Allah na wakamuomba Allah awasaidiye ndipo Allah alipo mtuma mtume wake kwa dini ya haki ili aishindishe juu ya dini zingine zote nae ndiye **Hadhrat Mirza ghulam Ahamd a.s** na ndiye anae timiza ile bishara ya mtume saw ya kuwa **THUMMA TAKUNU KHILAFAT ALAA MIN HAJ NUBUWAT**. Maana baada yake silsila ya ukhalifa ika anza na inaendelea hadi sasa tunavyo zungumza.

**Na atakayekufuru Baada ya hayo, basi hao ndiyo wavunjao Amri.** Hili ni onyo kwa waislam wote na onyo hili lilianza kuonekana mara tu baada ya Hadhrat Abubakar[ra] kuchukua kiti cha ukhalifa kuna waislam wakagoma kutoa zaka na wengine kwenda kinyume na amri za khalifa wa zama Mwenyezi Mungu alimsaidia na akashinda na wale waasi waka dhalilika sana kwa adhabu waliyo pata toka kwa Allah. Hata hivyo katika amri hii au maneno haya yanaonesha kwamba waislam wakiendelea kuasi au kuto fanya matendo mazuri basi neema ya ukhalifa haitakuwa pamoja nao, na badala yake itakuwa adhabu ambazo leo hii tunazishuhudia kwa wale ambao bado hawajamkubali Imam wa zama na ukhalifa wake wapo kwenye shida kubwa mno na moto una endelea kuwa wakia.

***Kitu kingine kinapatikana katika fungu hili ambamo aya ya ahadi ya ukhalifa inapatikana na biblia inasemaje.***

Kwanza tuanze na Biblia kwani inasema '' Biblia inasema '' Basi mtiini Mungu, zipingeni hila za shetani naye atawakimbia'' **[Yakobo 4:7]**

Hivyo Quran imekuja na fundisho kubwa zaidi na kuweka msisitizo mkubwa kwani sehemu nyingi ndani yake tumeamriwa kutii maagizo ya Mwenyezi Mungu. Hivyo katika fungu hili linalo zungumzia ahadi ya ukhalifa neno **Utii** limezungumziwa mara 7 saba kuonyesha kuwa ni nijambo la muhimu sana na ni namba witri yaani hiyo saba na yenye maana haigawiki kwa mbili na kumaanisha kuwa jambo la utii halina mwisho mwislam anatakiwa kuwa mtiifu sana bila kuchoka wala kujiuliza kwanini nitii.

Swala la utii limezungumzwa sana hata na mtume Muhamaad saw mwenyewe na Quran inatutaka tuendelee kumtii. Qurani inasema **mtiini Allah na mtume**. Pia inatwambia na anacho kupeni mtume chukueni, na anacho wakatazeni jiepusheni nacho [**Alhashir aya ya 8**] Hadithi moja mtume saw anasema **Mumtii kiongozi hata kama mnaona anakichwa kidogo kama cha tende.** Hapa tunaona msisitizo wa utii hivyo ni wajibu wa waislam kutii na hasa sisi tuliyo mkubali Imam wa zama.

*Itaendelea..... toleo lijalo Inshallah*

# Utengezaji wa Kashta za Ubuyu

Na **Mtandao**



**Mahitaji:**

- Unga wa ubuyu 1/2
- Sukari 1/4
- Rangi kijiko 1 cha chakula
- Vanilla kifuniko 1
- Maji vikombe 2
- Pilipi manga

**Jinsi ya kuzipika**

i. Chukua unga Wa ubuyu chekecha upate ule mzuri na safi.
ii. Kisha weka maji yako jikoni tia sukari, Rangi, vanilla na pilipili manga.
iii. Koroga mpaka uone mchanganyiko wako unatoa povu na ukigusa unanata.
iv. Weka unga wako, anza kusonga kama ugali hivi.
v. Andaaa sinia, paka mafuta epulia hapo kisha usukume na sukumio la chapati, kisha kata mtindo uupendao.

Furahia kashata za ubuyu.

## ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA$^{AS}$

### Kuwasingizia Wengine

Kusingizia na kunasibisha dhana mbaya juu ya matendo ya watu wengine ni maradhi na dhamira mbovu nafsini mwa mtu inayochafua uzuri wa imani yake na utawa na huiunguza kwa haraka kama vile moto uunguzavyo majani makavu. Zama wauguao maradhi hayo wawafanyapo Manabii shabaha za mashambulio yao na kuwasingizia, Mungu huwa adui wao Naye Huwalinda Manabii Wake. Hulinda heshima ya wapenzi Wake kwa ghera isiyo na kifani. Nilipozozwa na kushambuliwa kwa njia mbali mbali, ghera hiyo hiyo ya Mungu ikawa ngao ikajitokeza kunilinda.

(Roohani Khazain Jal. 20: Al-Wasiyyat Uk. 26 maelezo)

# Maadhimisho ya Ukhalifa

## Majlis Ansarullah, Tanzania

*Kutoka Uk wa 4..*

**na alifariki mwaka 644 tarehe 3 mwezi wa 11 katika mwezi wa dhul hijja akiwa na umri wa miaka 61.**

**Hadhrat Othman Bin Affan ra alianza kuongoza tarehe 6 novermber mwaka 644 hadi tarehe 17 June mwaka 656. Alizaliwa mwaka 576 kabla ya hijria na kufariki 17 June mwaka 656 katika mwezi wa dhul hijja akiwa na umri wa miaka 83.**

**Hadhrat Ali Bin Abii Twalib r.a aliongoza toka mwaka 656 hadi tarehe 28 mwezi January mwaka 661 akiwa na umri wa miaka 60.**

***3 Je katika zama za mwisho zipo ahadi zozote za uwepo wa khalifa.***

Naam katika zama za mwisho upo utabiri ambao Mtume Muhammad saw alibashiri uwepo wa ukhalifa chini ya kivuli cha unabii. Jambo hili linakubaliwa na wanazuoni wote wa kiislam na waislam kwa ujumla kuwa kuna zama zitakuja na mara nyingi wamehangaika kuuhuisha ukhalifa huo bila mafanikio kwa sababu wale wanao taka kuusimamisha ukhalifa wanakiondoa cheo cha unabii na kutaka ukhalifa ujitegemee na ni jambo lisilowezekena kwa mujibu wa kanuni za kibishara na dini kwa ujumla. Kwanza tuangalie ndani ya Quran Mwenyezi Mungu anatwambia nini **katika sura nnur 24 aya ya 56 kuwa Na Allah amewaahidi wale walioamini na kufanya vitendo vizuri katika ardhi Bila shaka atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya wale wa kabla yenu, Na kwa yakini atawaimarishia dini yao aliyowapendelea na atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Na atakayekufuru Baada ya hayo , basi hao ndiyo wavunjao Amri [sura nnur 24 aya ya 56]**

**Hapa kuna point kadhaa tuzieleze kwanza**

Sharti lakwanza watu wawe waaminio yaani walio mwamini Allah na mtume wake kisha wakafanya vitendo vizuri. Kwa hakika ni sharti walilopewa waislam ili wapate neema hiyo ya ukhalifa, na kwa hakika sharti hili lina walenga waislam moja kwa moja kwa sababu Allah ana wafananisha na wale wa kabla yao ambao walifanywa makhalifa wakati walipo mwamini Allah na wakafanya vitendo vizuri.

**Atawaimarishia dini yao aliyowapendelea.** Dini inayo zungumzwa hapa na Allah ni Islam kwasababu Allah anasema katika sura ya ٥ aya yake ya ٤ kuwa leo nimewakamilishieni dini yenu na kuwatimizieni neema yangu na nimewapendeleeni Islam iwe dini yenu. Sasa khalifa ambaye Mwenyezi Mungu anatoa ahadi kaziyake kuja kuimarisha dini hii ya Islam na sio dini nyingine. Hivyo waislamu wote wanatakiwa kufuata amri hii ili ahadi hii itimie kwao kwa sababu Allah kamwe Hatoi ahadi isiyo weza kutimia.

**Atawabadilishia Amani baada ya hofu yao,** kwanza kabisa tujue kuwa hofu huwa haipatikani wakati watu wako na Amani hofu huja pale kitu ukipendacho kikiondoka ghafla, mfano anapo fariki mzazi au mke au yule mtu ambaye katika maisha haya ya dunia mlishibana sana. **Hivyo kwa upande wa waislam masahaba r.**a walimpenda sana mtume Muahammad saw na walipo sikia amefariki tu wengine hawakuamini na kulia sana ,mfanno wao Hasan bin Thabit r.a mwingine Hadhrat Omar Bin Khattab r.a Mfano huu wa hadhrat Omar r. ulikuwa ule ambao unaonyesha jinsi gani alivyokuwa na khofu na hakujua afanye nini muda ule, ndipo Mwenyezi Mungu alipo muinua Hadhrat Abubakar swddiq r.a na kuwasomea aya inayo eleza kifo cha mtume na kuwaeleza anae mwabudu Muhammad ajue huyo amesha kufa na anaye mwabudu Allah basi ajue Allah yu mzima na Hafi. Hapo hofu walio kuwa nayo muda ule ikatoweka yote na Amani ikapatikana na islam ikaendelea kushinda chini ya kiongozi huyu yaani Hadhrat Abubakar r.a. **Sasa hofu ya pili inakuja kwetu sisi wa zama hizi kwakuona uislam unashambuliwa na waislam wamegawanyika na hatujui tuta jibu nini au tu ueleze na kuu safisha vipi Uislam na masingizio**. Walipatikana watu wachache wenye yakini kwa Allah na wakamuomba Allah awasaidiye ndipo Allah alipo mtuma mtume wake kwa dini ya haki ili aishindishe juu ya dini zingine zote nae ndiye **Hadhrat Mirza ghulam Ahamd a.s** na ndiye anae timiza ile bishara ya mtume saw ya kuwa **THUMMA TAKUNU KHILAFAT ALAA MIN HAJ NUBUWAT**. Maama baada yake silsila ya ukhalifa ikaanza na inaendelea hadi sasa tunavyo zungumza.

1 **Na atakayekufuru Baada ya hayo, basi hao ndiyo wavunjao Amri.** Hili ni onyo kwa waislam wote na onyo hili lilianza kuonekana mara tu baada ya Hadhrat Abubaka$^{ra}$ kuchukua kiti cha ukhalifa kuna waislam wakagoma kutoa zaka na wengine kwenda kinyume na amri za khalifa wa zama Mwenyezi Mungu alimsaidia na akashinda na wale waasi wakadhalilika sana kwa adhabu waliopata toka kwa Allah. Hata hivyo katika amri hii au maneno haya yanaonesha kwamba waislam wakiendelea kuasi

***Itaendelea..... toleo lijalo Inshallah***

# Jalsa Siiratunnnabiyy S.A.W Yaadhimishwa – Jamia Ahmadiyya Tanzania.

Na Mwandishi wetu

Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu s.w wanatawi wa Jamia Ahmadiyya walipata fursa adhwim ya kuadhimisha siku muhimu kabisa katika ulimwengu wa kiislam, hiyo ni siku ya siirat-un-nabii s.a.w. Dhumuni kubwa la kuadhimisha siku hii ni kuwakumbusha waislam historia, maisha, sera na khulka njema za mtume wetu mtukufu Muhammad[saw].

Maadhimisho hayo yalifanyika siku ya jumanne ya tarehe 6/06/2023 katika ukumbi wa chuo uliopo Kihinda mkoani hapa Morogoro.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo alikuwa Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhatti Sahib, Mkuu wa Chuo cha Jamia Ahmadiyya na naib Amir nchini. Hafla ilianza majira ya saa 4:00 asubuhi kwa usomaji wa Quran iliyosomwa na ndugu Husein Omari Mpenda na kufuatiwa na shairi la kiurdu ambalo lilisomwa na ndugu Hamim Walid Hamis.

Baada ya shairi hilo, ilifuata hotuba yenye anuwani isemayo, “Shauku ya Mtume mtukufu[saw] katika ibada ya Mungu mmoja.” Hotuba hiyo ilitolewa na ndugu Naim Andale ambaye alianza hotuba yake kunukuu aya ya 163 kutoka suuratul-An’aam [6:163] ambayo inasema: “Sema: Hakika sala yangu, na sadaka yangu, na uzima wangu na kufa kwangu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, mola wa ulimwengu.” Mzungumzaji alitoa mifano kadhaa kufafanua hotuba yake murua.

Baada ya hotuba hiyo ilifuata hotuba iliyochukua kichwa cha habari kisemacho, “Mapenzi ya maswahaba kwa Mtume mtukufu[saw]”, hotuba hiyo ilitolewa na Mwalimu Shamuni Mwishehe Juma. Mwalimu alianza hotuba yake kwa kunukuu aya ya 10 kutoka suratul-Hashr [59:10] ambayo inaeleza mapenzi makubwa waliyokuwa nayo maswahaba wenyeji wa Madina kwa ndugu zao waliohamia kutoka Makka akiwemo Mtume mtukufu[saw]. Kisha Mwalimu alisema kuwa maswahaba wa Mtume[saw] walimpenda kuliko hata kwa wazazi wao, wake au waume zao na ndugu zao wote. Aidha alitoa mifano kadha wa kadha kutoka katika matukio ya Badri, Uhudi, Khandaq n.k

Baada ya hotuba hiyo ilifuata hotuba yenye maudhui yasemayo, “Jinsi Mtume s.a.w alivyowatendea maadui zake na watu wa dini zingine.” Mada hii ilitolewa na Maulana Sheikh Shahab Ahmad Sahib. Sheikh Sahib alianza hotuba yake kwa kusoma aya ya 22 kutoka suratul ahzaab [33:22] isemayo kuwa: “Bila shaka mnao mfano mwema kutoka katika mtume wa Mwenyezi Mungu.




Baada ya kusoma aya hiyo, sheikh sahib alisema kuwa Mtume wetu mtukufu[saw] alipitia kila hatua katika maisha yake yote. Alipitia ujana, na utu uzima pia, alikuwa raia wa kawaida na baadaye akawa kiongozi mkuu kabisa, alikuwa mwajiriwa masikini na baadaye akawa tajiri, alikuwa mnyonge na baadaye akawa mtawala mwenye mamlaka juu ya wale waliomtesa hapo kabla. Katika hali hizo zote, Mtume[saw] alidumu kuonesha mifano bora kabisa ambapo hadi siku ya kiama hautapatikana mfano wake.

Sheikh sahib alitoa mifano kadhaa kama vile Mtume[saw] alivyowaruhusu wakristo wa Najran kufanya ibada yao katika msikiti wake wa Madinah, na mkataba wa amani aliowaandikia wayahudi, wazartashti na wakristo na mengine mengi ili kuonesha jinsi Mtume Mtukufu[saw] alivyowatendea watu wa imani na dini zote.

Baada ya hotuba hiyo ilifuata Qaswida ya kiarabu na kufuatiwa na hotuba katika lugha ya Kiurdu iliyokuwa na madhumuni isemayo: “Mfano mwema na subira ya Mtume Mtukufu[saw]. katika hali ya shida na mateso” Hotuba hiyo ilitolewa na Maulana Sheikh Ayyaz Ahmad dogar. Alieleza matukio kadhaa kutoka katika maisha ya Mtume wetu Mpendwa[saw]. yaliyoonesha jinsi alivyosimama imara katika hali ya shida na mateso.

Baada ya hotuba hiyo ilifuata hotuba iliyokuwa na madhumuni isemayo: “Shauku ya Mtume mtukufu[saw] katika kuhubiri umoja wa Allah.” Hotuba hiyo ilitolewa na Maulana Sheikh Karimuddin Shams Sahib, mbashiri wa mkoa wa Morogoro.

Katika hotuba yake Sheikh sahib alitaja mifano kadhaa kuthibitisha hamasa ya Mtume s.a.w katika suala la mahubiri.

Alisema Mtume[saw] aliwaita watu juu ya mlima Safaa, akaandaa karamu ya chakula mara kadhaa, kama haitoshi akaandika barua nyingi za kuhubiri wafalme wa nchi mbalimbali kama vile Rumi, Iran, Misri, Ethiopia n.k.

Baada ya hotuba hiyo, zilifuata nasaha chache za mgeni rasmi, yeye alisema kuwa kuhusu khulka njema ndio msingi imara wa mahubiri. Alisema kuwa Mtume[saw] alizishinda nyoyo za watu kwa njia hii tu na sio kwa silaha. Hivyo akawahimiza wahudhuriaji kudumisha khulka njema ili kupata mafanikio katika uwanja wa mahubiri. Mwisho Naib Amir Sahib aliongoza maombi ya kimya na kufunga kikao.

Kisha mgeni rasmi [Naib Amir Sahib] alianza kwa kusoma aya ya 5 katika Suratul-Qalam [68:5] inayosema kuwa: “Hakika wewe [Mtume s.a.w] una tabia njema, tukufu.”

# Falsafa ya Idul Adh’ha

*Kutoka uk. 7*

itahesabika lakini idadi vya Nabii Ibrahim haitahesabika. Utabiri huu kwa kweli ulimhusu Mtume Muhammad[saw] na muda wa kuenea kwa vizazi wa Nabii Ibrahim ni zama ya Mtume Muhammad[saw]. Hivyo, idi hii ni kumbusho la kujitolea kwa Nabii Ismail na ni ushuhuda kwamba neno la Allah lililoteremshwa kwa Nabii Ibrahim miaka elfu nne ya nyuma lilihusu ujaji wa Mtume Mtukufu[saw] na lilitimia kumpitia yeye tu. Kwa kupitia idi hii tunatangaza kwamba vizazi vya Nabii Ibrahim si watoto tu ambao aliwazaa bali wafuasi wote wa Mtume Mtukufu[saw] ni vizazi vyake vya kiroho.

**IDI HUJA BAADA YA KUJITOLEA MHANGA**

Hazrat Khalifatul Masihi wa Nne (ra) anasema:

Ipo dhana ya idi kila baada ya kujitolea mhanga. Sasa iangaliwe kwamba Nabii Ibrahim alipokamilisha kujitolea kwake basi idi yake ilikuwa idi ya maana kwelikweli. Atakuwa ameomba kwa Mola wake malipo makubwa ya kujitolea kwake. Ndiyo maana aliomba malipo yafuatayo:

Ewe Mwenyezi Mungu mimi ninapenda malipo ya aina moja tu ya haya yote nilijitolea mimi au watoto wangu au wajukuu zangu watakavyoendelea kujitolea; ya kwamba miongoni mwetu umwinue yule Mtume mwenye sifa kubwa ambaye uliwahi kuahidi na manabii yaani utupatie Mtume Muhammad[saw] kama zawadi. Hivyo, idi ya Mtume Mtukufu[saw] itakuwa idi ya kujitolea kwetu.

(Khutbat -e- Tahir, Hotuba za Idi, uk. 429)

**KUJITOLEA KWETU USHINDI WETU**

Hazrat Musleh Ma’ud (ra) akiwapa habari ya furaha wanajumuiya anasema:

“Madamu wanajumuiya wetu wataendelea kujitolea kwa ajili ya dini na madamu wataendelea kusonga mbele katika kujitolea sana kwa ajili ya dini ya Uislamu basi hata kama mataifa yote ya dunia na wafalme wote wa dunia wakijumuika pamoja hawawezi kutuangamiza katu. Allah subhanahu wataala alisema Hazrat Masihi aliyeahidiwa pia ni Ibrahim hivyo ninyi ni watoto wa kiroho wa Ibrahim huyo. Ndiyo maana, nyinyi ni jiwe kuu la pembeni mkidondoka juu ya yeyote ataangamia au kama mwingine atawashambulia; mwenyewe ataangamia.

(Khutbat-e-Mahmood, juz. 2, uk. 280)

# Kalamu kutoka Kanda ya Ziwa

*...Kutoka tolro lililopita*

**KUCHANUA KWA CHEMCHEM YA JAMAAT AHMADIYYA MKOANI SHINYANGA - 5**



*Yousuph Mgeleka (Muijukuu)*

Seyidna Ahmad anasema: “Nitaitanguliza dini mbele ya dunia”

Ndivyo ilivyotokea kwangu. Mwaka 2017 nikiwa jijini Daressalaam, nilipatwa maradhi fulani na kulazimika kufanyiwa upasuaji wa tumbo. Nikiwa katika wiki moja tangu kufanyiwa upasuaji, nikapokea simu ya kunijulia hali kutoka kwa maulana Sheikh Waseem Ahmad, ambaye alikuwa akiishi Mwanza lakini ndie alikuwa msimamizi wa mkoa wetu wa Shinyanga. Baada ya kunijulia hali Sheikh Waseem sahib alinijulisha kusudio la kufanyika tena mkutano wa Jalsa nyingine mkoani Shinyanga na kwamba walishakaa (wakati mie naumwa) na kukubaliana kuwa ifanyikie tawini Sungamile, nami nikamwambia ni muhimu sana Jalsa ifanyike na iendelee kufanyika. Japokuwa mie naumwa ila ningetamani tuwe sote.

Baada kama ya siku nne au tano hivi, nikapokea simu ya Amir sahib maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akinijulia hali, na mara baada ya hapo alinidokeza kusudio alilopokea kutoka mkoani kwangu Shinyanga kwamba tumedhamiria kufanya tena mkutano wa Jalsa Nau Mubaein. Nikamjibu ni sawa Amir sahib na ninazo taarifa zote, japokuwa mie nipo bado naumwa kwa kufanyiwa operesheni ya tumbo. Akanipa pole na kisha kuniombea du’a ya shifaa.

Kwa kipindi changu cha wiki mbili tangu nimefanyiwa upasuaji, nikapokea agizo la Amir sahib kwamba “Unatakiwa kuwepo mkoa wa Shinyanga na kuandaa mkutano wa Jalsa, na kwamba imebaki wiki moja mkutano kufanyika”. Tumefundishwa na Allah juu ya KUSIKIA NA KUTII, naam nikamkubalia Amir sahib na kumuhakikishia kuwa nitasafiri siku chache zijazo na nitafika kusimamia maandalizi ya Jalsa, nikamwambia usiwe na wasiwasi Amir sahib. Akanishukuru, pia akamjulisha na maulana Sheikh Waseem sahib juu ya ujio wangu mkoani Shinyanga.

Ndugu zangu ikumbukwe nilisafiri kwa gari nikiendesha mwenyewe kutoka Dar mpaka Kahama ambayo ni zaidi ya kilometa elfu moja, huku nikiwa namaumivu makali kwenye mshono tumboni na hasa ukaaji. Sikuwa na jinsi maana Amir sahib nakumbuka aliniambia kwenye simu kuwa “tunahofu sana ufaulu wa Jalsa iwapo hautakuwepo”, hii kauli ilinitafakarisha sana. Nikamwambia mke wangu mmoja juu ya safari yangu, naye akataharuki na kusema iweje usafiri wiki hizi mbili tatu tangu ufanyiwe upasuaji? Nikamwambia hili ni agizo la Amir sahib. Mke wangu huyo akapata wasiwasi mkubwa sana na kuniambia kwa nini usitafute dereva akusaidie, hivi utafika salama kweli? Nilimhakikishia na kumthibitishia kuwa nitasafiri na nitafika salama Kahama InshaAllah. Nakumbuka hata mama yangu mzazi ilimjia hofu kubwa sana, wote nikawahakikishia kuwa msiwe na wasiwasi ilimuradi naenda kufanya kazi ya Jamaat hivyo ondoeni shaka yoyote.

Kweli, nilisafiri. Na nilisafiri mwenyewe kwa kuendesha gari Dar mpaka Kahama. Nikaondoka Dar saa moja kamili asubuhi siku ya Jumapili, ambapo ilitakiwa (sawa na ratiba) jumapili inayofuata ndio iwe mkutano wa Jalsa pale Sungamile. Nilichokifanya, nikampigia simu khadim mmoja kijana aitwae Juma Ngate wa Sungamile aliyekuwa ameenda Zanzibar na ambae alishaniambia siku nikienda Kahama basi nimjulishe tuambatane.
Nikamjulisha nae akavuka na meli za usiku na alfajiri akawasili Dar, yeye nilisafiri nae kwa tahadhari tu nisiwe peke yangu kwa hali yangu ile, na uzuri khadim huyo alikuwa anapajua mpaka nyumbani kwangu Kahama, hivyo ikawa ni rahisi kwangu. Tulisafiri wote mpaka majira ya saa tano usiku tukafika Kahama salama kabisa Alhamdulillah, japokuwa safari yote nilijizuia kula zaidi ya kunywa vimiminika tu sawa na hali yangu. Nikiwa njiani safarini nakumbuka maulana Sheikh Waseem sahib alikuwa akinipigia kujua kama kweli nimesafiri na nimeondoka Dar, nikamjuza kuwa Alhamdulillah nipo safarini nae kuniombea pia

Siku iliyofuata yaani Jumatatu, nililazimika mimi na Sheikh tulikuwa na miadi kufanya mialiko kwa viongozi wakuu wa mkoa wa Shinyanga na hususan Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga. Tukafanya hivyo, nikasafiri tena kutoka Kahama mpaka Shinyanga mjini na tukatimiza hayo yote na nikampatia mrejesho kiongozi wetu Amir sahib maulana Sheikh Choudhry sahib. Baada ya hapo sasa ndio tukaanza hekaheka za maandalizi ya eneo pale Sungamile, mahemezi, matayarisho yote ya ukaaji na mapishi. Nakumbuka hali yangu kiafya nilikuwa na maumivu makali na hata kusimama wima nilikuwa siwezi kwa mshono kuvuta, waila sikuiacha kazi ya Jamaat.

Nikarudi Kahama nikiwa na Sheikh Wasim Sahib ambapo alilala Kahama pia. Kesho yake asubuhi aliondoka kurejea Mwanza nami kubaki na zoezi la mahemezi na matayarisho yote ya mkutano pale Sungamile, nikiwa ni Afsa Jalsa. Nikaanza kuunda kamati siku ya Jumanne hiyo nikiwa Kahama, nikawa nashinda Sungamile muda wote kuhakikisha yanaenda sawa nikishirikiana na marehemu Mwl Mohamed Namwete sahib na Rais wa Tawi mzee Shaaban Kalanga sahib. Huku nikiwa napita kwa wanajamaat kuwahamasiha sana kuelekea Jalsa, Alhamdulillah sote tukawa ni kitu kimoja. Pia tukaanza kupokea wageni kutoka maeneo mbalimbali ikiwemo wale waliotokea Daressalaam akiwemo Maulana Sheikh Ame sahib, Sadr Mbambwa sahib na Mwl Mbanga sahib wote wakatufikia. Tukawapokea.

Siku ya Jalsa ikawadia, nakumbuka jana yake (Jumamosi) sikuweza kupumzika na hata kulala sawa na hali yangu, huku maumivu makali yakinisibu nikivumilia. Kila kitu sawa uwezo aliotujaalia Allah vilikaa sawa, wageni wengi sana kutoka matawini walilala kwenye Jalsa Gah. Asubuhi tukazidi kupokea wageni, na majira ya saa mbili na nusu asubuhi tukapokea ugeni wa askari polisi wakafika Sungamile na kufanya ukaguzi kadhaa wa mazingira na mkao wake. Na muda huo wakanipatia taarifa kuwa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa Shinyanga anakuja kushiriki mkutano wenu kwa siku nzima, anakuja na Kamati yake nzima ya Ulinzi na Usalama. Na kwamba tuwe tayari kumpokea kuanzia saa nne kamili, kweli ikawa hivyo.

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa akawasili tawini Sungamile akiwa kwenye msafara wa magari zaidi ya 8, huku akiambatana na kamati yake ya Ulinzi na Usalama. Hakika ujio wake kwenye Jalsa yetu ukabadilisha muonekano na fikra za baadhi ya wenyeji wa kijiji hicho ambapo nao wakalazimika kufika na kushiriki mkutano wetu huo. Hakika ile Jalsa ya Sungamile ilifana sana na ushiriki ulikuwa ni mkubwa sana, hali njema ya utulivu ilitawala, na khutba nyingi kukonga nyoyo za wanajumuiya na washiriki wote. Jamaat mkoani Shinyanga kwa mara ya kwanza ikapata heshima ya kipekee. Yaani kutoka ule mkutano pale Tinde na mazingira yake, Allah akaiteremshia heshima Jumuiya yake na hapo ikazidi kutambulika zaidi na serikali nzima ya Mkoa wa Shinyanga na jamii kwa ujumla wake. Jalsa ikafana sana, matunda mema yakaonekana Alhamdulillah. Na hapo ikawa ni ufunguo mpana zaidi kwa Jamaat Ahmadiyya mkoani Shinyanga kuzidi kupanuka, matunda mema kuonekana.

Sisi ambao Allah ametujaalia kuzishuhudia nyakati zote tangu Jamaat inaanza mkoani Shinyanga, tukapata jingine la kujifunza. Mwenyezi Mungu anasema katika al Qur’an Sura Al-Dhuha “Walal aakhiratu khairu lakaminal uuwala – Nyakati zijazo ni bora kuliko zilizopita”. Ndio, maana kila nikikaa na kulinganisha ilivyokuwa ile Jalsa ya kwanza pale kijijini Tinde na changamoto zake, na nikilinganisha na hii ya Sungamile basi nikajionea tofauti ya neema kubwa sana ambayo Allah ametuteremshia sisi wafuasi wa Jumuiya yake. Ndipo nikazidi kujifunza kupitia ile Jalsa ya Tinde na mvua kunyesha mwishoni, kwamba hizi ndio neema ambazo Allah anaziteremsha kupitia Jalsa hii ya Sungamile. Ilikuwa ni ufaulu wa maajabu sana tawini Sungamile kupitia Jalsa Salana ile. Lakini nikajifunza pia, kupokea agizo la Amir wako na kujitoa muhanga kulitekeleza kikamilifu huku ukihatarisha hata afya yako kwa ajili ya Jumuiya yako, Allah akaja kuonyesha miujiza yake mikubwa. Ni watu wachache sana ndio waliojua kuwa mie nilikuwa ni Afsa Jalsa lakini nikiwa ni mgonjwa kabisa, na nilijitahidi sana kumeza dawa za maumivu ambazo zilinisaidi yeyote kutobaini iwapo nina operesheni.

Kwa ujumla wake hapa tunapata mafunzo kadhaa. Kwanza ni kumtegemea Allah na kuzitambua ishara zake njema kwetu kuhusu Jumuiya yake. Lakini pili tunajifunza namna ya kujitolea kwa kuitanguliza dini mbele ya dunia, na namna Allah anavyoweza kukusaidia na kukuvusha katika jambo ambalo wengi wanaadam wakijawa hofu, waila kwa Allah ni jambo jepesi sana. Na kwa kupitia tukio hili la mkutano wa Jalsa ya Sungamile iliniha sana kiimani na kumtegemea Allah kwa kila namna, na kwamba tunapomtanguliza Allah, naye hutusaidia pasipo hesabu.

Nakumbuka siku iliyofuata baada ya Jalsa kuisha, mpendwa wetu Amir sahib ilibidi afunge safari maalum na kuja kunitembelea nyumbani kwangu Kahama mjini. Alifunga safari ili kuja tu kunishukuru kwa kazi kubwa na nzuri kuifanikisha Jalsa Salana ya Sungamile kwa kiwango kikubwa mno, na namna ambavyo sikujali juu ya afya yangu bali ni kuitikia na kutekeleza wito na maagizo ya Amir sahib kikamilifu. Ndugu zangu, hii ndio ilikuwa mara yangu ya kwanza mimi kutembelewa nyumbani kwangu na Amir wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini.

Kumbe, huo ndio ukawa ni ufunguo rasmi kutoka kwa Allah. Kwamba kuanzia sasa, utatembelewa sana na muwakilishi wa Khalifa wa zama nyumbani kwako, yaani Amir wa nchi kukufikia nyumbani kwako. Na kweli Alhamdulillah, maana hivi sasa sijui hata idadi ya mara ngapi mpendwa kiongozi wetu Amir sahib amefika nyumbani kwangu, ni mara nyingi mno kufikiwa ugeni wa Amir wa nchi nyumbani kwangu huku bara, yote ni KUSIKIA NA KUTII pamoja na kuitanguliza dini mbele ya dunia. Alhamdulillah.

*Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo*

# Muhammad saw: Mfano Bora

*Kutoka uk. 12*

wa Maquraishi walikataa pendekezo hili kwa msingi kwamba kama Muhammad (saw) angeondoka Makka, Waislamu bila shaka wangekubali uamuzi wao na kuingia kwenye uwanja wa vita wakiwapinga. Katika tukio la Bai'at ya pili pale 'Aqabah, wakati suala la kuhama kwa Mtukufu Mtume (saw) lilipoibuka mbele ya Ansar wa Madinah, mara moja walisema, "Hii ina maana kwamba tunapaswa kuwa tayari kwa vita dhidi ya Arabia nzima."

Mtukufu Mtume (saw) alipoondoka Makka, alitupia jicho la huzuni kwenye mipaka ya Makka na akasema, "Ewe Makka! Ulikuwa mpenzi wangu kuliko miji mingine yote, lakini watu wako hawakuniruhusu kuishi hapa." Juu ya hili, Hadhrat Abu Bakr (ra) akasema, "Wamemfukuza Mtume wa Mwenyezi Mungu. Sasa hakika wataangamizwa. "

Kwa mukhtasari, kwa muda wote Mtukufu Mtume (saw) alipoishi Makka, alistahimili kila aina ya mateso, na kamwe hakuchukua upanga dhidi ya Maquraishi. Sababu ikiwa ni kwamba kwanza, kabla ya hatua zozote kuchukuliwa dhidi ya Maquraishi, kwa mujibu wa desturi ya Allah, ujumbe wa Mwenyezi Mungu ulihitaji kuwasilishwa bayana, na hili lilihitaji muhula.

Pili, pia ilikuwa ni matakwa ya Mwenyezi Mungu kwamba Waislamu waonyeshe kielelezo cha msamaha na subira hadi ule ukomo wa mwisho ambapo baada ya hapo kukaa kimya ilikuwa ni sawa na kujiua, jambo ambalo haliwezi kuchukuliwa kuwa ni tendo la kupongezwa na mtu yeyote mwenye akili timamu.

Tatu, Maquraishi waliongoza aina ya serikali ya kidemokrasia huko Makka na Mtukufu Mtume (saw) alikuwa mmoja wa raia wake. Kwa hiyo, uraia mwema ulidai kwamba kwa muda wote Mtukufu Mtume (saw) alipobaki Makka, aheshimu mamlaka, na asiruhusu chochote ambacho kingeweza kuvuruga amani, na suala hilo linapovuka kikomo cha msamaha, yeye ahame kutoka hapo.

Nne, ilikuwa ni lazima pia kwamba mpaka watu wake wawe wanastahiki adhabu kutokana na matendo yao katika makadirio ya Mwenyezi Mungu, na mpaka pale ambapo muda wa kuwaangamiza haujafika, Mtukufu Mtume (saw) aishi miongoni mwao, na wakati huo ulipofika, naye afikie kuhama kutoka huko. Sababu ikiwa ni kwamba, kwa desturi ya Allah, muda wote ambapo Mtume wa Mwenyezi Mungu atabaki ndani ya watu wake, hawapigwi na adhabu ambayo ingewaangamiza. Wakati adhabu ya kuangamiza inapokaribia, Mtume anaamrishwa kuondoka mahali hapo. Kutokana na sababu hizi, kuhama kwa Mtukufu Mtume (saw) kulikuwa na dalili tofauti ndani yake, lakini inasikitisha kwamba watu hawa watenda maovu hawakutambua, na waliendelea kukua katika dhulma na uonevu wao. Kwani lau kuwa Maquraishi wangejiepusha hata wakati huo, na wakaacha kulazimisha maswala ya dini, na wakawaruhusu Waislamu kuishi maisha ya amani, basi Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa rehema kuliko wanaorehemu, na Mtume wake pia. Rahmatullil-'Alamin. Hakika hata hivyo wangesamehewa. Hata hivyo, maandishi ya amuzi la kimbingu yalipaswa kutimizwa. Kuhama kwa Mtukufu Mtume (saw) kulitumika kama kuni juu ya moto wa uadui wa Maquraishi na walisimama kwa hamasa na ghasia kubwa zaidi kuliko hapo awali, ili kuufuta Uislamu.

Pamoja na kuwatesa na kuwadhulumu Waislamu masikini na wanyonge, ambao mpaka sasa bado walikuwa Makka, kazi ya kwanza ya Maquraishi, mara tu walipogundua kwamba Mtukufu Mtume (saw) ameondoka Makka, ni kwamba walitoka nje ya mji kumfuata. Walichunguza kila inchi ya Bonde la Bakkah, wakimtafuta Mtukufu Mtume (saw) na hata kufika kwenye mdomo wa pango la Thaur. Hata hivyo, Allah Aliyetukuka alimsaidia Mtukufu Mtume (saw) na akaweka pazia juu ya macho ya Maquraishi, kwamba baada ya kufika mahali pale walipofikia, walirudi wakiwa wamechanganyikiwa na bila mafanikio. Walipokatishwa tamaa na utafutaji huo, walitoa tangazo la wazi kwamba mtu yeyote ambaye angemrudisha Muhammad saw - akiwa amekufa au yuko hai - angepokea zawadi ya ngamia mia moja, ambayo ni sawa na takriban Rupia 20,000 katika sarafu ya leo.

Huzur (atba) alieleza kwamba hii ilikuwa thamani wakati ambao Hadhrat Mirza Bashir Ahmad (ra) aliandika kitabu hiki. Leo, hiyo itakuwa sawa na makumi ya mamilioni ya pauni.

Vitisho vya Maquraishi Dhidi ya Waislamu

Khalifa mtukufu (atba) aliendelea kunukuu, "Vijana wengi kutoka katika makabila mbalimbali ya Maquraishi walitoka kila upande kumtafuta Mtukufu Mtume (saw) kwa uchoyo wa zawadi. Kwa hivyo, ufuatiliaji wa Suraqah bin Malik, ambao tayari umetajwa katika Juzuu ya I ya kitabu hiki, pia ulikuwa ni matokeo ya tangazo hili la malipo. Hata hivyo, Maquraishi walifanywa kukabiliana na kushindwa katika mpango huu pia. Mtu akitafakari, ili vita izuke kati ya mataifa mawili, hata sababu hii pekee inatosha, kwa kuwa zawadi ya namna hii imewekwa kwa ajili ya Mwalimu na Kiongozi wa wengine. Vyovyote iwavyo, mpango huu ulipoonekana kutofaulu na Maquraishi wakagundua kwamba Mtukufu Mtume (saw) amefika Madinah akiwa salama salimini, kama ilivyotajwa hapo juu, wakuu wa Maquraishi walituma barua ya vitisho vikali kwa mkuu wa Madinah, 'Abdullah bin Ubayy bin Sulul, na viongozi wenzake.

"Umemlinda mtu wetu (yaani, Muhammad (saw) na tunaapa kwa jina la Allah kwamba utamwacha na kumpiga vita, au kwa uchache kabisa, utamfukuza kutoka mji wako. Kama sivyo, bila shaka tutakusanya jeshi letu lote na kukushambulia; na tutawauwa wanaume wenu na kuwachukua wanawake wenu katika milki yetu wenyewe, tukijihalalishia sisi wenyewe.

Wasiwasi ambao ungeweza kuwasakama maskini Muhajirin kutokana na barua hii unadhihirika, lakini mtetemeko wa hofu pia ulienea kupitia Ansar pia. Mtukufu Mtume (saw) alipopata habari hizi, alikwenda kwa Abdullahh bin Ubayy mwenyewe. Mtukufu Mtume (saw) alijadiliana naye na kumtuliza akisema: "Hakika jamaa na ndugu zako wako pamoja nami, je, utapigana na wapenzi wako mwenyewe?" Ilikuwa katika siku hizi ambapo Sa'd bin Mu'adh (ra), mkuu wa Aus, alikuja Makka kwa ajili ya 'Umrah. Alipomuona, macho ya Abu Jahl yalichuruzika damu kwa hasira na akasema kwa hasira, "Umempa ulinzi muasi yule (Muhammad (saw). Unaamini kuwa utaweza kumlinda...?" Katika zama hizi, Maquraishi walikuwa wamejishughulisha sana na kuing'oa Islam hivi kwamba wakati Walid bin Mughirah, chifu wa Makka alipokaribia kufa, alianza kulia bila kizuizi. Watu waliuliza juu ya mateso yake, na akajibu, "Naogopa, dini ya Muhammad (saw) isije ikaenea baada ya kufa kwangu." Viongozi wa Maquraishi wakamjibu kwa kusema, "Asiwe na wasiwasi, tunamhakikishia kwamba hatutaruhusu dini yake kuenea. Matukio yote haya ni baada ya kuhama, wakati Mtukufu Mtume (saw) alipoondoka Makka, akiwa amehuzunishwa na mateso ya Maquraishi, na inaweza kudhaniwa kwamba Maquraishi wangewaacha Waislamu kwenye hali yao.

Si hayo tu, bali Maquraishi walipoona kwamba Aus na Khazraj walikataa kuacha ulinzi wao kwa Mtukufu Mtume (saw), na ikachukuliwa kwamba Islam inaweza kukita mizizi katika Madinah, walitembelea makabila mengine ya Arabuni na kuanza kuyachochea dhidi ya Waislamu. Kwa vile Maquraishi walikuwa na ushawishi wa kipekee juu ya makabila mengine ya Arabuni, kutokana na ulezi wao wa Ka'bah, kwa sababu hii, kwa ushawishi wa Maquraishi, makabila mengi yakawa maadui wabaya wa Waislamu. Hali ya Madinah ilikuwa kana kwamba imezingirwa na moto mkali. Na hivyo, riwaya ifuatayo tayari imetajwa:

"Ubay bin Ka'b (ra) ambaye alikuwa miongoni mwa Maswahaba mashuhuri anasimulia, 'Wakati Mtukufu Mtume (saw) na Maswahaba zake walipohama kwenda Madinah, na Ansar wakawalinda, matokeo yake Uarabuni yote kwa pamoja ikasimama dhidi ya Waislamu. Katika zama hizo, Waislamu hawakuvua hata silaha zao wakati wa usiku na wakati wa mchana walikuwa wakitembea huku na huku wakiwa na silaha endapo itatokea shambulio la ghafla. Wangeambiana kwamba tuone kama tutaishi hadi wakati ambapo tunaweza kulala kwa amani usiku bila hofu yoyote isipokuwa kumcha Mungu.'"

Hali ya Chifu wa Wanadamu mwenyewe ilikuwa kwamba:

"Hapo mwanzo, Mtukufu Mtume (saw) alipofika Madinah, mara nyingi alikuwa akikaa macho wakati wa usiku kwa kuogopa mashambulizi ya adui.

Kuhusiana na zama zile zile, Kurani Tukufu inasema:

"Na kumbukeni mlipokuwa wachache mkionekana wadhaifu katika ardhi, mkawaogopa watu kuwanyang'anyeni, lakini Yeye akawapeni makao na kuwasaidieni kwa msaada Wake na kuwapeni vitu vizuri ili mpate kushukuru." (8:27)

Hii ilikuwa ni hali ya vitisho vya nje na, hata katika Madinah, hali ilikuwa kwamba mpaka sasa, sehemu kubwa kutoka miongoni mwa Aus na Khazraj ilisimama kidete juu ya ushirikina. Ingawa inaonekana walikuwa pamoja na ndugu zao na jamaa zao, lakini katika mazingira kama hayo, mshirikina angewezaje kuaminiwa?

Pili, walikuwepo wanafiki, ambao hapo mwanzo walikuwa wameikubali Islam, lakini kwa siri walikuwa maadui wa Islam, na kuwepo kwao Madinah kulileta uwezekano wa vitisho.

Tatu, walikuwepo Wayahudi, ambao ingawa kulikuwa na mkataba nao, lakini kwa Wayahudi hawa thamani ya mkataba huu haikuwa kitu. Kwa hiyo, kwa namna hii, kulikuwa na vipengele hivyo vilivyokuwepo hata katika Madinah yenyewe, ambavyo vilikuwa si chini ya hifadhi ya risasi zilizofichwa dhidi ya Waislamu. Cheche ndogo ya makabila ya Waarabu ilitosha kuwasha risasi hizi moto, na kuwaangamiza Waislamu wa Madinah kwa mlipuko mmoja.

Katika wakati huu wa hatari, ambao ulikuwa wakati wa hatari zaidi haujawahi kuwazukia Waislamu hapo kabla, wahyi wa Mwenyezi Mungu ulitumwa kwa Mtukufu Mtume (saw), kwamba sasa yeye pia achukue upanga dhidi ya makafiri hawa, ambao waliingia katika uwanja wa vita dhidi yake, upanga mkononi, kwa njia ya dhulma na jeuri tu. Kwa namna hii, Jihad kwa njia ya upanga ilitangazwa."' (The Life & Character of the Seal of Prophets Vol II uk. 54-60).

Mara ya Kwanza Jihadi ya Upanga Kuruhusiwa

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba kwa mujibu wa utafiti wa Hadhrat Mirza Bashir Ahmad (ra), aya ya kwanza kuhusu Jihadi kwa upanga iliyoteremshwa kwa Mtukufu Mtume (saw) ilikuwa tarehe 12 Safar mwaka wa 2 Hijiria. Imenakiliwa pia katika baadhi ya riwaya kwamba aya hii iliteremka wakati wa kuhama, kwani Mtukufu Mtume (saw) alikuwa ameanza kutuma wajumbe kwa ajili ya ulinzi wa Madinah dhidi ya vitisho vya kweli. Kwa vyovyote vile, hii ilikuwa ni mara ya kwanza kabisa kwa Mtukufu Mtume (saw) kupewa ruhusa na Mwenyezi Mungu kuchukua upanga ili kujilinda dhidi ya dhulma mbaya na ukatili ambao ulikuwa ukifanywa juu yake. Aya ya Quran iliyoteremshwa kuhusiana na jambo hili ilikuwa:

"Imeruhusiwa (kupigana) kwa wale wanaopigwa, kwa sababu wamedhulumiwa; na kwa yakini Allah Anao uwezo wa kuwasaidia;

Waliotolewa majumbani mwao pasipo haki ila kwa sababu tu wanasema: Mola wetu ni Allah. Na kama Allah Asingaliwazuia watu, baadhi yao kwa wengine, bila shaka yangalivunjwa mahekalu na makanisa, na nyumba za ibada na misikiti ambamo jina la Allah hutajwa kwa wingi. Na bila shaka Allah Humsaidia yule anayemsaidia Yeye; hakika Allah ni Mwenye nguvu, Mshindi;" (22:40 - 41)

Khalifa mtukufu (atba) amesema kuwa hii haikuwa tu kwa ajili ya kuwalinda Waislamu, bali kwa kuzitaja sehemu za ibada za dini nyinginezo, aya hii pia inalinda haki na uhuru wa dini nyingine pia.

Mikakati Minne Iliyowekwa Wakati wa Uadui Dhidi ya Waislamu

Huzur (atba) zaidi amemnukuu Hadhrat Mirza Bashir Ahmad (ra) ambaye anaandika mikakati minne ya mwanzo iliyotumiwa na Mtukufu Mtume (saw):

KWANZA: Mtukufu Mtume (saw) alianza kusafiri kuyaendea makabila ya jirani na kufanya mapatano ya amani nao, ili eneo linaloizunguka Madinah lisiwe na tishio. Katika suala hili, Mtukufu Mtume (saw) alitilia maanani maalum yale makabila ambayo yalikuwa karibu na njia ya biashara ya Syria ya Maquraishi. Kwa kadri kila mtu anavyoweza kutafakari, yalikuwa ni makabila haya hasa, ambayo kwayo Maquraishi wa Makka wangeweza kupata manufaa zaidi dhidi ya Waislamu na ambao uadui wao ungeweza kusababisha vitisho vikali kwa Waislamu.

PILI: Mtukufu Mtume (saw) alianza kutuma makundi madogo madogo ili kupata taarifa za kijasusi katika pande tofauti kutoka Madinah, ili aweze kuwa na habari za mienendo ya Maquraishi na washirika wao; na Maquraishi pia waelewe kwamba Waislamu hawakujisahau, ili kwamba kwa namna hii, Madinah ingeweza kulindwa kutokana na hatari za mashambulizi ya ghafla.

TATU: Busara nyingine ya kupeleka vikundi hivi ilikuwa ni ili Waislamu wanyonge na masikini wa Makka na maeneo ya jirani wapate fursa kwa njia hizi, kujiunga na Waislamu wa Madinah. Hadi sasa, kulikuwa na watu wengi katika eneo la Makka ambao walikuwa Waislamu moyoni, lakini hawakuweza kukiri hadharani imani yao katika Islam kutokana na ukatili wa Maquraishi. Zaidi ya hayo, kutokana na umaskini wao na udhaifu wao, hawakuweza kuhama pia, kwa sababu Maquraishi wangewazuia kwa nguvu watu kama hao kuhama.

NNE: Mbinu ya nne aliyoitumia Mtukufu Mtume (saw) ni kwamba alianza kuizuia misafara ya wafanyabiashara ya Maquraishi iliyokuwa ikisafiri kutoka Makka kwenda Syria ikipitia Madina njiani. Sababu ikiwa ni kwamba kwanza, misafara hii ingezua moto wa uadui dhidi ya Waislamu popote walipokuwa wakisafiri. Ni dhahiri kwamba kwa mbegu ya uadui kupandwa katika viunga vya Madinah, ilikuwa ni hatari sana kwa Waislamu. Pili, misafara hii ingekuwa na silaha kila wakati na kila mtu anaweza kufahamu kwamba kwa misafara hiyo kupita karibu na Madinah haikuwa isiyo ya hatari. Tatu, riziki ya Maquraishi kimsingi ilitegemea biashara. Kwa hiyo, katika mazingira haya, njia ya uhakika na yenye ufanisi zaidi ambayo kwayo Maquraishi wangeweza kutiishwa, ukatili wao ungeweza kukomeshwa, na wangeweza kusukumwa kwenye mapatano, ilikuwa ni kwa kuizuia njia yao ya biashara.

Kwa hivyo, historia inashuhudia ukweli kwamba miongoni mwa mambo ambayo hatimaye yaliwalazimu Maquraishi kuelekea kwenye mapatano, utekaji nyara wa misafara hii ya biashara ulikuwa na nafasi muhimu sana. Kwa hivyo, huo ulikuwa mkakati wa busara sana, ambao ulizaa matunda ya mafanikio kwa wakati ufaao. Nne, mapato yatokanayo na misafara hii ya Maquraishi yalitumika zaidi katika juhudi za kuuondoa Uislam. Bali, baadhi ya misafara ilitumwa kwa madhumuni ya pekee ili faida yao yote itumike dhidi ya Waislamu. Katika hali hii, kila mtu anaweza kuelewa kwamba kutekwa kwa misafara hii kwenyewe, kulikuwa kwa haki, na halali kabisa.'The Life & Character of the Seal of Prophets Vol II uk. 90-92).

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba mada hii itaendelea katika hotuba zijazo.

Sala ya Jeneza

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba ataongoza sala ya jeneza ya wafu wafuatao:

Khawaja Muniruddin Qamar kutoka

***Endelea uk. 3***

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

# Mapenzi ya Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

# Muhammad saw: Mfano Bora

'Maisha ya Mtukufu Mtume (saw) : Mazingira Yaliyopelekea Vita vya Badr'

Baada ya kusoma Tashahhud, Ta'awwuz na Surah Al-Fatiha, Khalifa Mtukufu, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (atba) alisema kwamba maisha, matukio na mihanga ya maswahaba walioshiriki katika Vita vya Badr yalishafafanuliwa kwa kina katika mfululizo wa hotuba. Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba wanajamaat wengi wamemweleza kwamba maisha ya Mtukufu Mtume (saw) yanapaswa pia kuelezewa kwa kina kwa sababu ilikuwa ni kutokana na kushikamana naye tu ndipo Maswahaba walipata vyeo vya juu. Hawakuamini tu bali walidhihirisha Umoja wa Mwenyezi Mungu kama walivyofundishwa na Mtukufu Mtume (saw).

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba kwa miaka mingi, ameangazia vipengele mbalimbali vya Mtukufu Mtume (saw) katika hotuba zake. Walakini, maisha yake yalikuwa hivi kwamba hayawezi kubanwa kwenye nyanja fulani pekee. Sifa zake zilikuwa na upana sana kiasi kwamba hata haziwezi kuzungumzwa katika hotuba kadhaa. Hivyo, maisha yake yataendelea kutajwa, kwa hakika, kila hotuba au mada inajumuisha kutajwa kwa kipengele fulani cha maisha ya Mtukufu Mtume (saw) kwa sababu maisha yetu yanazunguka kwake. Hatuwezi kutenda kwa mujibu wa Shariah bila ya mfano wake.

Hali Zilizopelekea Vita vya Badr

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba leo ataanza mfululizo wa hotuba kuhusu Mtukufu Mtume (saw) kuhusiana na Vita vya Badr. Kabla ya kutaja vita vyenyewe, Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba ni muhimu kuelewa mazingira ambayo yalisababisha vita kutokea hapo kwanza. Huzur (atba) alimnukuu Hadhrat Mirza Bashir Ahmad (ra) ambaye aliandika:

Maisha ya Makka ya Mtukufu Mtume (saw), ukatili waliofanyiwa Waislamu na Maquraishi na njama walizozitumia ili kuufuta Uislamu, zilikuwa sababu tosha ya kuzuka vita baina ya makundi mawili, kila zama, na katika aina zote za hali. Historia inathibitisha kwamba pamoja na dhihaka za kudhalilisha sana, na kejeli na kashfa za kuudhi kupita kiasi, makafiri wa Makka waliwazuia kwa nguvu Waislamu kumwabudu Mungu Mmoja na kutangaza Umoja Wake. Walipigwa kikatili sana na kuteswa bila huruma, mali na alipatwa na kila aina ya mateso. Kwa kulitaja jina la Mwenyezi Mungu tu, marafiki na wapambe wa Maquraishi walimpiga Mtukufu Mtume (saw) kwa mawe huko Ta'if, kiasi kwamba mwili wake ulilowa damu. Hatimaye, kwa makubaliano ya wawakilishi



*Hadhrat Ameerul Mumineen Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa Tano[atba] akihutubia waumini katika Masjid Mubarak, Uingereza siku ya Tarehe 2 Februari 2023, Muhaamad; Mfano Bora.*

zao zilinyang'anywa kinyume cha sheria, walisusiwa kama njia ya kutaka kuwaua na kuwaamgamiza, huku wengine wakiuawa shahidi bila huruma huku wanawake wao wakivunjiwa heshima. Hii ilikuwa ni kwa kiasi cha kusikitisha sana na kwa ukatili huu Waislamu wengi waliondoka Makka na kuhamia Abyssinia. Hata hivyo, Maquraishi hawakutulia katika jambo hili pia na wakatuma wajumbe kwenye Baraza la Kifalme la Negus kwa kujaribu ili kwamba Muhajirin hawa kwa namna fulani wangerejea Makka na Maquraishi wangefaulu katika kuwageuza kutoka katika imani yao, au kuwaua.

Kisha, maumivu makubwa yaliwekwa juu ya Bwana na Kiongozi wa Waislamu, ambaye alikuwa kipenzi zaidi kwao kuliko nafsi zao, wote wa makabila mbalimbali ya Maquraishi, iliamuliwa katika Bunge la kitaifa la Makka kwamba Muhammad (saw), Mtume wa Allah, auwawe ili athari zote za Uislamu zipate kufutiliwa mbali, na Umoja wa Mungu uweze kukomeshwa. Kisha, ili kutekeleza kwa vitendo azimio hili la umwagaji damu, vijana wa Makka waliotoka katika makabila mbalimbali ya Maquraishi, walikusanya kundi na kushambulia nyumba ya Mtukufu Mtume (saw) usiku. Hata hivyo, Mwenyezi Mungu alimlinda Mtukufu Mtume (saw), na akaondoka nyumbani kwake - akiwaacha katika butwaa - na akajificha kwenye pango la Thaur. Je, ukatili huu na maazimio ya umwagaji damu hayakuwa sawa na tangazo la vita kutoka kwa Maquraishi?

Kwa nyuma ya pazia ya matukio haya, je, mtu yeyote mwenye akili timamu anaweza kudai kwamba Maquraishi wa Makka hawakuwa na vita na Islam na Waislamu? Basi je, ukatili huu wa Maquraishi haungeweza kuwa sababu za kutosha za kuhalalisha vita vya kujihami kwa Waislamu? Je, katika mazingira kama haya, taifa lolote lenye kujiheshimu duniani na ambalo halijaamua kujiua, lingeweza kubaki nyuma kutokana na kukubalika kwa uchokozi kama huo uliofanywa na Maquraishi juu ya Waislamu? Kwa hakika kabisa, kama kungekuwa na taifa jingine badala ya Waislamu, wangeingia kwenye uwanja wa vita dhidi ya Maquraishi mapema zaidi. Waislamu, hata hivyo, waliamrishwa waonyeshe subira na msamaha na Kiongozi wao.

Kwa hivyo, imeandikwa kwamba wakati mateso ya Maquraishi yalipozidi, Abdur-Rahman bin 'Auf (ra), na Masahaba wengine, walijitokeza mbele ya Mtukufu Mtume (saw) na kuomba ruhusa ya kupigana na Maquraishi, lakini Mtukufu Mtume (saw) akajibu:

"Kwa sasa, nimeamriwa kusamehe. Hivyo, siwezi kukupeni ruhusa ya kupigana."

Kwa hivyo, Maswahaba walivumilia kila maumivu na matusi katika njia ya dini, lakini hawakuacha kushikilia subira. Wakati kikombe cha mateso ya Maquraishi kilipojaa na kuanza kufurika; na Mungu wa ulimwengu huu akaona ujumbe wa Mwenyezi Mungu umefikishwa kwa ukamilifu, hapo ndipo Mungu alipomwamuru mtumishi wake aondoke katika mji huo. Kwa sasa, jambo hilo lilikuwa limevuka kikomo cha msamaha, na wakati ulikuwa umefika ambapo wahalifu wangefikia mwisho wao mbaya. Hivyo, kuhama huku kwa Mtukufu Mtume (saw) kulikuwa ni ishara ya kukubalika kwa kauli ya mwisho ya Maquraishi. Ilikuwa ni dalili ya maamuzi ya Mungu ya tangazo la vita; Waislamu na makafiri walielewa hili.

Hii ndiyo sababu, wakati wa mashauriano pale Darun-Nadwah, wakati mtu mmoja alipopendekeza kwamba Mtukufu Mtume (saw) afukuzwe kutoka Makka, wakuu

*Endelea uk.11*




J. D. Shams

Maulana Jalalud-Din Shams alizaliwa mwaka 1901. Alipata hati ya H. A. (Honours in Arabic) katika Punjab University na pia alihitimu kozi ya kuwa Mbashiri wa Kiislamu na akapata shahada kutoka katika Jamia Ahmadiyya, Qadian.

Mnamo mwaka 1925 akawa Mbashiri Mkuu wa Jumuiya za Waislamu katika nchi za Mashariki ya Kati kwa miaka 7 hivi.

Katika mwaka 1936, Khalifatul Masih wa Pili r.a. alimpeleka London akiwa Mbashiri Mkuu wa Jumuiya za huko ambako alitumikia sana dini hadi vita kuu ya pili.

Mnamo mwaka 1946 alirejea kwenye Makao Makuu ya Jumuiya Ahmadiyya, Qadian, na akapewa madaraka ya kuwa msimamizi wa mahubiri nchini India na baada ya Pakistan kuzalika akaendelea na cheo hicho hicho nchini Pakistan hadi 13 Oktoba 1966 ambapo alifariki dunia.

Alipata kuandika vitabu 40 katika lugha ya Kiingereza, Kiurdu na Kiarabu. Alitetea sana dini ya Kiislam maishani mwake, hadi Khalifa wa Pili r.a. alimpatia lakabu ya "Khalid".

YESU KAFIA WAPI? - J. D. Shams

YESU KAFIA WAPI?



J. D. Shams

**Je, Wajua?**

Je wajua sawa na mipango ya kampuni binafsi za anga, kufikia mwaka 2030 kutakuwa na space tourism (utalii wa angani) na watu watakuwa wakienda sehemu mbali mbali angani kutaliii, mfano kutalii katika mwezi.

Nakala hii itapatikana kwa Sh. 2,900/=


Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com